Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Wale walioamini na ikatulia mioyo yao kwa kumkumbuka Allah. Sikilizeni! Kwa kumkumbuka Allah mioyo hutulia.
(Ar-Ra'd 13:29)

JUZU 79 No. 202 | RAJAB-SHA'BAN 1439 AH | APRILI 2019 | SHAHADAT 1398 HS | BEI TSH. 500/=

Islam: Dini Ilokamilika

Na **Sheikh Ahmad Daudi**
Jamia Ahmadiyya Tanzania



Hii ni mada muhimu sana kwa kuwa inahusiana na maisha ya mwanadam yeyote, mada muhimu kwa sababu kutokana na maelezo yake wasomaji watayafahamu mambo mbalimbali katika mafundisho ya dini ya Islam na watatambua jinsi Uislam unavyotoa mchango wake katika kutatua matatizo mbalimbali hususan ya maisha yetu ya leo yanayoyoyumba kama bahari yenye tofani.

Tukianzia na neno Islam, maana yake ni **mfumo wa maisha unaofuata amri na sheria ya Qur`ani Tukufu** na maana yake ni **kunyenyekea na kutii**. Pia lina maana ya **Amani**. Mwislamu ambaye ni mtu anayefuata mfumo huu wa maisha, ananyenyekea na kutii kwa Mola wake kwa kuwa ndiye aliyemuumba. Lakini ni lazima kwake kuidumisha Amani kwa viumbe wengine wa Allaah, wakiwemo wanadamu, wanyama, ndege, wadudu na viumbe wengine kwa kumuogopa Allah tu.

Dini ni **ustarabu wa maisha wanaoufuata watu katika kuonyesha utii wao kwa kile wanachokiabudu**. Na kukamilika ni kutimia kwa kitu, kikawa hakina upungufu wala kasoro. Hivi dini ya Islamu imekamilika kwa sababu katika Qur'an Tukufu, Allah Ametangaza wazi kuwa dini ya Islamu imekuja kukamilisha mlolongo wa dini zote za nyuma yake kwa kuwa na mafundisho makamilifu. Na kwamba kama vile Mwanadamu alivyopita katika hatua kadhaa za mabadiliko ya kimwili (physical evolution) hadi kufikia hatua aliyo kuwa nayo leo, ndivyo alivyopita katika mabadiliko ya kiroho (spiritual

Endelea uk. 3

Mbeya Waadhimisha Siku ya Masihi Aliyeahidiwa

Na **Mwandishi Wetu**



Mnamo tarehe 24/3/2019 Mkoa wa Mbeya uliadhimisha siku ya Masihi Aliyeahidiwa as sambamba na mkutanjo wa amani uliowakutanisha zaidi ya watu 165 wakiwemo wafanya kazi wa serikali, maafisa, maustadhi, maprofessa, walimu wa shule, viongozi wa dini mbalimbali na wafuasi wa madhebu mbalimbali wa dini tukufu ya Islam n.k.

Hotuba mbili za ufunguzi zilitolewa tokea upande wa Jumuiya ya Ahmadiyya na Sheikh wa mkoa mwenyeji, Sheikh Karimuddin Shams kisha Sheikh Abid Bhatti ambaye ni Mkuu wa Jamia Ahmadiyya Tanzania akamalizia.

Hotuba ya kwanza upande wa wageni ilitolewa na

Endelea uk. 8

Mvuleni Yang'arishwa

Na **Twahira Swalehe Kapilima**



Siku ya Jumapili, tarehe 7 April 2019 Lajna Imaillah Kitonga (kina mama wa Kiahmadiyya) walifanya Waqal Amal ya nguvu katika zahanati ya serikali ijulikanayo kwa jina la Mvuleni. Matawi hayo ni Jalsa Gah, Kitonga, Qadian na Sekondari ya Ahmadiyya. Yote hayo ni matawi ya Kitonga.

Lajna hao walifanya shughuli hiyo ikiwa ni kutimiza sehemu ya wajibu wa kiimani kwani sawa na Hadithi ya Mjumbe wa Allah saw (usafi ni sehemu ya imani).

Jumla ya washiriki 59 walihudhuria katika zoezi hilo wakiongozwa na Marais wa matawi yao.

Kaba ya kwenda zahanatini hapo washiriki hao walikutana Jalsa

Endelea uk. 8

Nilivyojiunga na Ahmadiyya Uk. 5

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Kila Ugonjwa....

Kijana wetu Jamil Iddi Mwanga alipata fursa ya safari ya kikazi nchini Japan na aliporudi tulipata wasaa wa kuzungumza naye. Katika mazungumzo hayo ambayo yalikuwa marefu lipo jambo ambalo taifa letu linatakiwa liweze kulizingatia.

Kijana huyo alitueleza kuwa Wajapani ni wachapa kazi kweli kweli. Hawana masihara hata chembe. Wanaheshimu kazi lakini pia waajiri wao wanawajali. Hili ni jambo la msingi katika maendeleo ya nchi. Jambo jingine ambalo kwa hakika ni mali yetu sisi Waislam ni kusoma. Hakuna anayeweza kubisha kuhusu hili. Jambo hili jema alikutana nalo kila mahali alipokwenda. Huku kwetu ukiingia kwenye treni utakuta wengi wamejiinamia na simu zao wakitazama vitu ambavyo heshima haituruhusu kuvitaja. Alililoliona Japani akiwa katika treni ni kwamba kila msafiri alikuwa ameinama katika kitabu chake akisoma. Hakuna makelele au mabishano.

Na hivi leo Japan ni moja ya nchi tajiri duniani. Lakini ukiona vyaelea vimeunda. Sisi kilichotusibu katika Afrika nini? Kumbuka Japan ni kisiwa. Afrika tunayo ardhi kubwa na yenye rutuba lakini tunasubiri mchele kutoka Japan. Tuna hospitali na tumewasomesha vijana wetu, tunazitumia hospitali hizo na tunahakikisha zina vifaa? Rasilimali zetu zinaishia katika mikono ya wajanja wa Ulaya. Nini kimetusibu Afrika?

Jibu la swali hili linapatikana katika kauli tatu zilizotolewa na Makhalifa watatu wa Masihi Aliyeahidiwa - Hadhrat Mirza Bashir-ud-din Mahmud Ahmad^{ra}, Hadhrat Mirza Nasir Ahmad^{rh}, Hadhrat Mirza Tahir Ahmad^{rh} na Hadhrat Mirza Masroor Ahmad atba.

Hadhrat Mirza Bashir-ud-din Mahmud Ahmad^{ra} alizungumzia ufagiaji wa takataka zilizoletwa na wakoloni za kuaminisha Waafrika kwamba hawakuwa na uwezo wa kufanya chochote. Mwana Aliyeahidiwa alisema hakuna watu walionyimiwa vipaji na Waafrika wana historia iliyotukuka iliyowafanya wawapokee Masahaba wa Mtukufu Mtume Muhammad^{saw}. Kinachotakiwa ni kuondoa kasumba ya kikoloni na kujenga kujiamini. Na hatua ya kwanza ni kuwa na lugha yetu wenyewe. Hakuna lugha mpya inayoweza kuwaunganisha watu wa bara hili kama Kiswahili. Hatua zimeanza kuchukuliwa za kuenzi Kiswahili lakini tunatakiwa tukimbie kwani kwa sasa tunatambaa.

Khalifa wa tatu, Hadhrat Mirza Nasir Ahmad^{rh} kwa vitendo alionyesha umuhimu wa elimu bora na sio bora elimu kwa kujenga shule na kutoa huduma za afya Afrka Magharibi. Ni kwa kiasi gani tumetilia mkazo wa elimu katika Afrika? Je elimu tunayoitoa inasaidia katika kutukomboa au inazidi kutudidimiza? Elimu hiyo ina uhusiano na mapambano yetu ya kujenga utu wetu uliobomolewa na utumwa, ukoloni na ukoloni mambo leo? Bila kutanzua suala la elimu Afrika inawezaje kupiga hatua ya kwenda mbele?

Khalifa wa nne, Hadhrat Mirza Tahir Ahmad^{rh} anakemea utumiaji mbaya wa rasilimali za Afrika. Anataka rasilimali hizo ziwe kwa manufaa ya wanachi wote. Je katika Afrika sote tunakula mezani au kama wale wanaosubiri makombo yaliyoanguka kutoka mezani? Ugawaji wa rasilimali ni jambo la msingi katika kuleta maendeleo ya jamii.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad atba amewakumbusha viongozi kuwa na hofu ya Allah na kutambua kuwa uongozi ni amana na kiongozi anatakiwa kuwa mtumishi na sio bwana.

Kila ugonjwa una dawa. Dawa ya Afrika ni kufuata ushauri wa viongozi hao watukufu wanaopata muongozo kutoka kwa Allah.

Hongera Mzee Sultan Wamwera

Katika Gazeti letu la ***Mapenzi ya Mungu*** toleo la mwezi Februari, 2019 kuna Makala yenye kichwa cha habari "Wamwera Atukumbusha" makala iliyoandikwa na Mzce Khamisi Sultani Wamwera. Baada ya kusoma makala hiyo nimeamua kuandika mistari michache kumpongeza Mzee Khamisi Sultani Wamwera kwa kazi kubwa na ngumu sana aliyoifanya.

Makala ya Mzee Wamwera imetudhihirishia na kututhibitishia wazi sisi Wanajumuiya wapya na Wanajumiya wa zamani kuwa tunayo hazina kubwa yenye elimu ya kuhifadhi kumbukumbu na matukio mbalimbali ya Jumuiya Ahmadiyya nchini Tanzania kupitia Mzee Wamwera. Kwa kweli sio kazi rahisi kukumbuka matukio mbalimbali ya Jumuiya Ahmadiyya yaliyotendeka nchini, kukumbuka majina ya watu mbalimbali waliojiunga na Jumuiya Ahmadiyya miaka ya 1955, ukilinganisha na umri mkubwa alionao Mzee Wamwera.

Mwisho namaliza makala yangu hii fupi kwa kumpongeza sana sana Mzee Khamisi Sultani Wamwera na hapo hapo namuombea kwa Mwenyezi Mungu amjaalie malipo yaliyo bora na akubali juhudi na huduma yake. AMINA.



MWANDISHI,

JUMANNE RAJABU
AHMADIYYA JAMAT
MOROGORO.

Chombo Madhubuti Ni 'Safina Ya Nuhu'

Na **Twahira Swalehe Kapilima**

Nimesoma kwa makini gazeti la ***Mapenzi ya Mungu*** toleo la Machi 2019 uk. 5, mada isemayo "***Tumia Chombo Hiki Usalimike***". Kwa kweli mwandishi amejitahidi sana kueleza kwa ustadi mkubwa jinsi ya kusalimika kwenye safari ya kutoka duniani kuelekea peponi kwa kutumia chombo kilichotengenezwa kwa:- Injini – *Sala*, Magurudumu – *Kuhiji Makka*, Usukani – *Zaka*, Taa – *Sadaka*, Nauli – *Shahada*, Kituo – *Msikiti*, Mkata tiketi – *Malaika* na tiketi yenyewe ni *udhu*.

Ukisoma kwa makini utagundua kuwa chombo cha usafiri tok duniani kuelekea peponi anachozungumzia mwandishi ni kutekeleza nguzo tano za Kiislam.

Nionavyo mimi ni kuwa nguzo tano pekee haziwezi kumfikisha msafiri peponi. Kwa maneno mengine kusafiri kwa kutegemea chombo hicho pekee safari itakuwa ya mashaka. Hivyo pamoja na kutumia chombo hicho muhimu, msafiri atalazimika kupanda '***Safina ya Nuhu wa zama hizi***'. Chombo hicho ni madhubuti kabisa kwani kimeundwa kwa idhini ya Allah mwenyewe. Nahodha wake Ameteuliwa na Allah^{sw}. Mwenye mapenzi makubwa na Allah^{sw} na Mtume saw. Mfafanuzi bora wa kitabu chake (Qur'an Tukufu). Mtetezi wa dini ya Allah^{sw} 'Islam'. Mwenye kujua maana halisi ya jihadi. Ndiye Isa. Ndiye Krishna. Muuaji wa nguruwe na mvunjaji wa msalaba. Mfundishaji wa jinsi ya kutekeleza haki za Allah na haki za viumbe wake na mambo mengine mengi. Kifupi amefundisha jinsi ya kumuabudu Allah.

Hivyo basi msafiri anatakiwa awe tayari kukubali fedheha na maumivu kwa ajili ya Allah. Atangulize dini juu ya dunia. Awe mtii kwa nidhamu ya Ukhalifa. Awe tayari kujitolea muda, maisha, mali kwa ajili ya Allah. Afanye mahubiri, aepukane kabisa na kiburi na majivuno. Adumu katika Durud Sharif. Mambo hayo yote na mengine atakayoamrishwa na Imamu wa zama awe kuyatekeleza. Imamu wa zama zetu kwa sasa ni Khalifatul Masih V, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad^{atba}.

Kuamini na kutekeleza yatolewa na Khalifa wa zama pia ni kutekeleza Masharti ya Baiat. Bali atakuwa pia ametekeleza nguzo sita za imani. Kwani atakuwa anaelewa kuwa Allah anaendelea kuongea hata sasa, Malaika wanaendelea kushusha Wahyi. Pamoja na kuamini vitabu Vyake atakuwa anaamini Qur'an Tukufu imehifadhiwa toka kale hadi sasa kwani hakuna aya zilizofutwa kama wanavyoamini baadhi ya watu. Mitume wasiokuwa na sheria mpya wataendelea kushushwa. Sheria ya mwisho ndiyo ile iliyoletwa na Mtukufu Mtume Muhammad^{saw} pia ndiye Khatam Nabiyyin. Msafiri wa chombo hiki atakuwa mbali na ushirikina, atakuwa amesimamisha umoja wa Allah.

Nimetanguliza kusema kuwa nje ya Safina ya Nuhu wa zama zeti hizi safari itakuwa ya mashaka kwa sababu wapo wengi wasio Waahmadiyya, kuna haja gani ya kuamini Mtume mwingine kwa natekeleza nguzo tano na vile vile nimeamini nguzo sita za imani.

Hivyo basi chombo alichoandika mwandishi ni kile ambacho Mwislam yeyote anakitumia tena kwa bidii sana kwa baadhi ya wasafiri. Kwa bahati mbaya anakosa nahodha.

Alhamdulillah thumma Alhamdulillah Allah Katuletea Imamu huyu, Masihi Ma'ud Mirza Ghulam Ahmad, Imam wetu wa zama. Nahodha wetu ndani ya Safina.

Allah Ametudumishia Ukhalifa toka 1908. Allah Mtukufu Aendelee kuulinda Ukhalifa. Tujitahidi kufuata maamrisho yote ya Allah yatolewayo na Imam wa zama. Tudumu katika kutekeleza masharti ya Ba'iat. Tumtii na kumuombea Khalifa wetu Hadhrat Mirza Masroor Ahmad^{atba}.

Allah Atujaalie tuwe waja wema, wenye khulka njema. Tusafiri salama kwenye safina yetu. Amin.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Islam: Dini Ilokamilika

Kutoka uk. 1

evolution). Mwanadamu huyu, historia inasema amekuwapo tangu wakati wa kipindi cha (palacocene) miaka 70,000,000 (sabini million) iliyopita (Guiness Book of World records). Lakini baada ya mabadiliko mengi ya nyuma kwa miongo kadhaa hajapata mabadiliko yeyote. Jambo hili linaonyesha kuwa Mwanadamu hatabadilika tena. Mabadiliko yake ya kimwili yamekamilika. Kwa utaratibu ule ule Mwenyezi Mungu Akakamilisha mabadiliko ya kiroho kwa kuteremsha Qur`an Tukufu yenye mafundisho yaliyokamilika.

Kama nilivyokwisha gusia mafundisho ya dini ya Islamu yanahusu maisha yote ya mwanadamu. Kama mifano tutatazama baadhi tu ya mafundisho machache.

UMOJA WA WALIMWENGU

Dini ya Islamu inafundisha kuwa binadamu wote ni sawa na wana haki sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Qur`an Tukufu inasema:

"*Enyi watu hakika tumewaumbeni katika kiume na kike, na tumewafanyeni mataifa na makabila ili mjuane, hakika aheshimiaye zaidi mbele ya Allah ni yule amchaye zaid katika ninyi*: (49:14).

Sawa na Aya hii hakuna mwanadamu ambaye ni mbora kuliko mwenzake mbele ya Mwenyezi Mungu tu. Kama ilivyo hali ya mwili, hali ya kiroho,Qur`an Tukufu inatangaza wazi wazi:

"*Na tulimtuma mtume katika kila umati (kuwaambia) mwabuni Allah na jiepushen na sheitani* (16:37).

Sawa na Aya hii Mwenyezi Mungu Anaweka utaratibu wa kidini katika kila taifa kwa kupitia wawakilishi wake ambao ni Manabii na hakuna taifa linaloweza kujitangazia kupendelewa katika neema hii. Hivyo ni makosa kuwa na fikra kwamba Waisraeli au watu wowote wale kuwa ni taifa teule. Katika sehemu nyingine Qur`an Tukufu inasema:

"*Tuliwatuma Mitume kabla yako, miongoni mwao wapo baadhi tulikuhadithia (habali zao) na wengine hatukukuhadithia*"(40:19)

Hivyo dini ya Islamu haina madai kama dini zingine kuwa Mitume wa kweli ni wale tu waliokuja kati yao. Bali inafurahia pale linapopatikana tangazo la uvumbuzi wa Nabii fulani katika jamii mbalimbali ulimwenguni ambao watu wana Imani kuwa walikuja kusimamisha maadili mema. Lakini zaidi ya hayo dini ya Islamu inakwenda hatua moja mbele zaidi na kutangaza kuwa wale wote wanaosimama imara katika mafundisho mazuri ya wateule hawa waliokuja kabla ya Mtume*saw* katika jamii mbalimbali hao wamepata ufaulu wa maisha yao kwa wakaa wao. Qur`an inasema;

Hakika wale walioamini na mayahudi na masabii na wakristo atakaye muamini Allah na siku ya mwisho na kufanya vitendo vizuri basi hao hawatakuwa na hofu wala hawatahuzunika (5:70)

Neno sabii katika aya hii inawahusu wale wote waliowahi kupata uongozi wa kiroho. Hivyo yeyote atakayejitahidi kuendana na mafundisho yao atakuwa ameokoka. Tazameni fundisho hili la ajabu la dini hii ambalo halipo katika dini nyingine yeyote ulimwenguni. Kila mmoja anadai kuwa wokovu uko kwenye dini hiyo tu. Kwa mfano waraka wa Papa kutoka Vatican umetangazwa kuwa wokovu ni mali ya Kanisa Katoliki na makanisa mengine ni batili na ni ya uongo. Viongozi kama hawa hawana imani kuwa Mungu kama anavyonyesha mvua yake bila kubagua ndivyo anavyonyesha mvua yake ya kiroho. Isitoshe ni tangazo la kanisa moja dhidi ya makanisa mengine, je, wale ambao hawana mnasaba na Ukristo Papa anafikira gani juu yao? Basi imani hii iliyoganda kwenye vilindi vya makanisa haitaruhusu umoja wa makanisa wanaoutafuma wafuasi wao. Umoja wa kimataifa umo katika Uislamu peke yake kwa sababu unakubali usawa wa wokovu na wema wa walimwengu wote.

UHUSIANO NA WATU WA DINI ZINGINE

Mfano wa pili ni fundisho la Islam juu ya kuwa na uhusiano mwema na watu wa dini zingine. Fundisho hili lipo hivi :- "*Allah hakuwakatazeni wale ambao hawakupigana nanyi kwa ajili ya dini wala hawakuwafukuzeni katika Nyumba zenu yakwamba muwafanyie hisani na adili hakika Allah huwapenda wafanyao uadilifu*" (60:9). Katika Aya hii dini ya Islam inawahimiza wafuasi wake kuwafanyia wema na ukarimu na kuwa na uhusiano mwema na watu wote ambao hawana uadui wa aina yeyote na hasa wa kuhatarisha maisha yao.

Fundisho hili limekaziwa zaidi katika Aya ifuatayo:

"Na uadui wa watu usiwashawishini kwa sababu waliwazuiweni msikiti uliokatazwa ya kwamba muruke mipaka. Na saidianeni katika wema na utawa wala msisaidiane katika dhambi na uasi. Na mwogope Allah. Hakika Allah ni mkali wa kuadhibu"(5:4). Katika Aya hii fundisho linasema sio suala la watu wengine wasio na kosa, bali hata wale wenye uadui wa namna fulani ni wajibu kuwafanyia uadilifu.

MAHUBIRI MAZURI NA UHURU WA MAONI YA DINI

Mfano wa tatu ni njia za mahubiri na anayehubiriwa anavyopewa uhuru wa maoni yake bila ya kulazimishwa kwa lolote. Qur`an Tukufu juu ya mahubiri inasema: *Uite (watu) kwenye njia ya Mola wako kwa hekima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa njia iliyo bora. Hakika Mola wako Ndiye Humjua sana aliyepotea katika njia Yake naye ndiye Awajuaye sana walioongoka*"(16:126)

Mahubiri yanatakiwa kufanywa kwa uangalifu mkubwa, hekima na maneno mazuri ni sharti muhimu. Na hoja ziwe zile zinazoathiri vizuri wala zisiwe zile zinazoleta chuki na uhasama. Kama Qur`an Tukufu inavyosema, sehemu nyingine.

"*Uzuie ubaya kwa yaliyo bora; Sisi Tunajua wanayoyaeleza*." (23:97). Kama wale wanaohubiriwa hawakubaliani na yale wanayohubiriwa badala yake wanayakataa, Qur`an inafundisha:-

"*Na kama wakigeuka, basi hatukukupeleka uwe muhifadhi wao,si juu yako ila kufikisha*" ikiwa Mwislam amefikisha ujumbe wa Islamu kwa njia ya mahubiri lakini akakataliwa anatakiwa aridhike kama ameshafikisha ujumbe wa Allah. Na si vinginevyo. Na kwamba hata kama jawabu la wanaohubiriwa ni matusi na kashfa, Qur`an inafundisha: "*Naye amekwishawateremshieni katika kitabu ya kwamba mnaposikia aya za Allah zinakataliwa na kufanyiwa mzaha, basi msikae pamoja nao mapaka waingie katika mazungumzo ghairi ya hayo maana mtakapo kaa pamoja nao mtakuwa kama wao. Hakika Allah Atawakusanya wanafiki na makafiri wote katika jahanamu*."(4:141)

Aya hii inamtaka Mwislam anayehubiri anapojibiwa kwa kashfa na matusi kama hana hoja ya busara basi afadhali aondoke sehemu hiyo. Hata kurudisha mashambulizi ya kashfa na matusi vilevile imekatazwa.

Wala msiwatukane wale ambao wanawaita kinyume cha Allah wasije wakamtukana Allah kupita kiasi bila kujua. Hivyo tumewapambia kila watu vitu vyao, kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola wao Naye Atawaambia yale waliyokuwa wakiyatenda. (6:109). Mbele ya mafundisho haya mazuri ni makosa makubwa kwa Waislam kuhusika na mahubiri yenye vurugu na yanayohatarisha amani. Lakini ni dhuluma kubwa kwa kanisa kushambulia dini ya Islam kuwa inatumia mabavu kuhubiri. Na hasa kanisa Katoliki. Maana historia iliyoandikwa na wao wenyewe inatisha na mtu mwenye roho ndogo damu humsisimka na pengine roho kukaribia kutoka kutokana na mambo yanayotisha yaliyomo katika historia hiyo. Na haya yote yalifanywa kwa sababu ya kukosa moyo wa uvumilivu na kusamehe wapinzani walio hitilafiana nao.

Ukizama nyuma katika historia jinsi Ma-papa wa kanisa Katoliki, maaskofu, na wakubwa mbalimbali walivyotumia upanga wa moto, kwa kuua watu waliohitilafiana nao kiitikadi, kwa kuwachinja, kwa kuwachoma wakiwa hai, na mateso mengine ya kila namna, kwa kuwatosa majini, kwa mamia na maelfu, mtu anashangaa. Kweli Bwana Yesu anasema kweli: *kwa nini unatoa kibanzi kilichomo kwenye jicho la ndugu yako wakati wewe mwenyewe una boriti machoni mwako.* Kweli nyani haoni kundule. Watu waliouwawa hivi na kanisa kwa sababu za kidini ni zaidi ya 50,000,000. Habari hizi zinapatikana katika vitabu vifuatavyo :-

1 *Historians History of the word* J.8 uk.352
2 *Encyclopaedia of religions and Ethics, habari za Inquisition*
3 *Buck`s Theological Dictionary and Peresecutions.*
4 *Osund`s Kingdom etc* uk. 107-133.
5 *Dawling`s History of Romanism*
6 *Fox Book of Martyrs.*
7 *Charlate Elizabeth`s Martyrology.*
8 *The War of the Huguenotes.*
9 *The Great Red Dragon.*
10 *Histories of the Reformation.*

Kuna mfano wa uvumilivu wa Mtume wa Islam Muhammad*s.a.w*, Abdullah bin Ubbay bin salul alikuwa adui mkubwa wa Islamu na maisha ya Mtume. Huyu ndiye aliyekuwa amewachorea maadui mipango ya namna ya kuwashambulia Waislam Madina. Katika sura ya (63:9) kimesimuliwa kisa ambapo wakiwa wanarudi katika vitani bwana huyu alisikika akisema: hivi karibuni watu wenye heshima watawafukuza watu dhalili kutoka Madina. Kila aliyesikia alielewa kuwa alikuwa akimlenga Mtume*s.a.w* watu wakakasirika sana. Na waliamini kuwa hatua kali ingechukuliwa

Endelea uk. 4

Islam: Dini Ilokamilika

Kutoka uk. 3

dhidi yake. Kwa kuwa kila mtu alikuwa na uhakika huo, Mtoto wa Abdullah akamwomba Mtume amruhusu kama anatoa adhabu ya kuuawa Baba yake, basi amuue yeye na si mtu mwingine ili asije akapata wazo la kulipiza kisasi. Mtume*saw* akakataa, si yeye wala mtu mwingine aliyeruhusiwa kumpa bwana huyu adhabu hata ile ndogo. Huu ni mfano mdogo tu wa jinsi bwana huyu alivyomuona Mtume*saw* dhalili na kumtukana matusi mabaya na njama zingine kubwa kubwa. Walipo wasili Madina Abdullah bin Salul hakukaa muda mrefu akafariki. Mtume*saw* alitoa nguo yake ili iwe sanda kwa ajili yake. Maswahaba ilibidi kushangaa kwa nini Mtume*s.a.w* amjali mtu huyo ambaye ni adui wa Uislam. Baada ya maandalizi ya mazishi kukamilika Mtume*s.a.w* akamsalia na kwenda makaburini kumzika. Wanao kashfu Uislamu waonyeshwe mifano mizuri ya namna hii ili kashfa na tuhuma zao ziwe za kweli, lakini watapata wapi, ambapo historia yao imejaa uozo. Na haitazamiki (habali hizi zimesimuliwa na Ibn Ishaq katika kitabu cha Seerat-un-Nabii cha Ibn Hisham sehemu ya tatu uk, 155). Pia sahihi Bukhari, kitabul Janaiz, BaabulFitan uk.96-97)

DEMOKRASIA YA KIISLAMU

Fundisho la nne na la mwisho kwa mada hii ni mfumo wa serikali unaopatikana katika mafundisho ya dini ya Islamu. Toka mwanzo ifahamike kuwa Uislamu hauna mfumo maalumu wa kiutawala ambao unaona kuwa ndio sahihi. Msimamo wake juu ya jambo hilo ni kwamba serikali yeyote iliyo madarakani ikawa inakubaliana na mila, desturi ya wananchi kwa jumla kwa kuonyesha ridhaa ya kuipenda, serikali hiyo ni halali. Si lazima iwe ya kidemokrasia kwa maana hii ya kuwa imechaguliwa kwa ridhaa ya wananchi kwa kura. Maana serikali za nchi nyingi huchaguliwa kwa njia hii lakini nyingi kati ya hizi hushindwa kabisa kupata sifa ile ya serikali ya kidemokrasia sahihi. Maana demokrasia sawa na maelezo ya Rais wa zamani wa marekani ni "*Government of the people by the people for the people*". Serikari zote zinafuzu kupata sifa mbili za mwanzo, yani zinakuwa ni serikali za watu si za viumbe tofauti, zikawa zimewekwa madarakani kwa njia ya kura. Lakini zikashindwa kutekeleza yale wanayo yahitaji wananchi. Kwa maana hiyo silazima kwa kila serikali iliyochaguliwa kwa njia ya kura iwe ni ya kidemokrasia sawasawa. Linaloonekana ni kuwa zaidi manufaa yanakuwa ni ya viongozi na wananchi hujikuta wakikabiliwa na shida na matatizo ya kila kukicha. Demokrasia yetu ya leo itakubaliwa na dini ya Islamu kama shart la tatu litatimia la wananchi kupata nafuu fulani ya maisha.

Misingi mikuu ya demokrasia ya Kiislamu ni miwili:

1: Watu wanaochagua wawe na imani ya kweli na yule au wale wanaowachagua na watambue kuwa yule anayechagua ingawa swala la kupiga kura ni hiari yake lakini hiari hii iko chini ya dhamana ya Mwenyezi Mungu na hivyo ni lazima azingatie dhamana hii kumpa mtu/watu wanaostahili watakaojali hali za wananchi na si hali zao tu. Kama kura hii atapewa mtu asiyestahili na wananchi kujikuta katika matatizo basi na yeye atahesabiwa kwamba amechangia katika shida za wananchi.

Mwenyezi Mungu anasema: *Hakika Allah Anawaamuruni kuzirudisha amana kwa wanaozistahiki* (4:590). Lakini kwa upande wa viongozi wanaochaguliwa Uislamu pia umewapa mambo yanayotakiwa kuyazingatia.

Hapa viongozi wanatakiwa kuonyesha uadilifu katika kuendesha masuala ya uongozi. Viongozi waachane kabisa na upendeleo kwao wenyewe, ndugu zao au marafiki zao. Na uongozi nao ni dhamana kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mtume*s.a.w* akakazania katika hadithi. Mfano mzuri wa kuwajibika kwa viongozi upo katika zama za uongozi wa khalifa wa pili wa Mtume*s.a.w* Seyidna Umar.

Yeye alikuwa na kawaida ya kuzunguka mitaani usiku bila ya kujitambulisha ili kufahamu shida za wananchi yeye mwenyewe. Siku moja katika pitapita yake akasikia kilio cha watoto toka mbali. Akahisi bila shaka kutokana na huzuni iliyogubika kilio kuna shida kubwa. Akaelekea upande wa kilio. Alipofika jirani akawauliza wenyeji wa mtaa ule kulikoni. Akaambiwa kulikuwa na mama mmoja pamoja na watoto watatu waliketi karibu na jiko lililo injikwa chungu wakingojea chakula. Akaenda hadi kwenye jiko hilo. Akamuuliza mama yule kuna tatizo gani ?

Akajibu watoto wangu wana njaa ya muda mrefu. Mimi sina chakula cha kuwapa. Nimeinjika chungu ambamo ndani yake nimetia maji, na kuendelea kuyachemsha. Kwa uchungu Seyidna Umar akageuza farasi wake. Akaenda haraka kwenye hazina kuu. Akachukua unga wa ngano, mafuta, nyama na tende akaweka ndani ya mfuko akamwambia mtumishi weka amtwishe begani. Mtumishi akamjibu: Bwana mkubwa usipate shida mimi nipo! Nitwishe nikusindikize niufikishe unakokwenda. Umar akajibu; la hasha, hapana shaka unaweza ukabeba mzigo wangu huu leo, lakini siku ya kuja onana na Mola wangu ni nani atakaye nibebea? Alikuwa na maana ya suala la shida za wananchi ni mzigo wake na ataulizwa yeye mbele ya Mwenyezi Mungu. Ni nani ataweza kujibu badala yake? Utawala wa aina yeyote wa mtu yeyote awe Mwislamu au asiwe Mwislamu kama kweli utakuwa na sifa ya kuwa na uchungu na kuguswa na shida za wananchi hiyo ni serikali inayokubalika Kiislamu. **Ni upuuzi kusema kuwa mtawala ni lazima awe Mwislamu.** Kwani yule mtawala wa Abyssinnie-Ethiopia ya sasa alikuwa Mwislamu? Yule alikuwa Mkristo lakini sifa zake zimejaa katika Qur`an Tukufu. Lakini serikali za aina hii ni muhali kuziona.

Mwisho Mwenyezi Mungu afunue macho ya walimwengu ili waone mafundisho haya ambayo kwa sababu ya kutimia faida zake imetimia katika sifa zake.

Mwenyezi Mungu atusaidie. Amina.

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA

Namna ya Kumuomba Mungu:

"mnaposali sala zenu, msiombe dua zenu kwa maneno ya Kiarabu tu kama watu wenye kughafilika; kwani sala zao na kutubia kwao hakuna maana. Lakini ninyi mnaposali si vibaya kuomba dua zenu kwa unyenyekevu katika lugha zenu isipokuwa Qur'an ambayo ni maneno ya Mungu na dua zilizobainishwa katika hadithi ambazo ni maneno ya Mtume, amani ya Mungu juu yake, ili alama ya kuomba na unyenyekevu iwe katika mioyo yenu."

(Safina ya Nuhu, uk. 92)

SHURA YA KITAIFA 2019

Amir Sahib - Jamaat Ahmadiyya Tanzania, anapenda kuwakumbusha Masheikh wa Mikoa, Marais wa Mikoa, Marais wa matawi, Walimu wa Jamaat nchini na Wanajumuiya wote kwa ujumla kwamba sawa na Kalenda ya matukio ya Jumuiya ya mwaka 2018/19, Majlis Shura ya Kitaifa itafanyika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga - Dar es Salaam, siku za Jumamosi na Jumapili tarehe 27 - 28 Aprili 2019.

Matawi yote yanatakiwa yafanye vikao vya kupendekeza ajenda za Shura pamoja na kuchagua wajumbe wa kuyawakilisha matawi yao kwenye Shura hiyo ya Kitaifa. Tawi lililo na wachangiaji zaidi ya 50, linaruhusiwa kuchagua mjumbe wa ziada kwa kila wachangiaji 50 wanaoongezeka.

Marais wote wa mikoa wanatakiwa washiriki. Pamoja na mjumbe wa Shura atakayechaguliwa kutoka kila tawi, Rais wa tawi naye pia anatakiwa ashiriki kwenye Shura ya mwaka huu.

Wajumbe wote wanatakiwa wawe wamefika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga Dar es Salaam jioni ya siku ya Ijumaa tarehe 26 Aprili 2019.

Ni muhimu kila tawi la Jumuiya lisipoteze nafasi yake ya kuleta mjumbe pamoja na ajenda kama watakuwa nayo.

Nilivyojiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya



Na

Musa

Abeli

Mbawala

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehema Mwingi wa Ukarimu

Kwa heshima na uaminifu wangu juu ya Jumuiya ya Ahmadiyya Tanzania nimeona niandike mambo machache ambayo Mungu wa Rehema Amenionyesha katika ndoto. Kabla sijaandika habari hizo naomba niseme jambo ambalo nahitaji msaada kutoka chumba cha uchapishaji kwa ajili ya kuweka vizuri maandishi yenyewe.

Pili, kama mtu atataka kuuliza swali lolote nitajibu mimi mwenyewe. Wala asisumbuke mtu mwingine. Asipate usumbufu wa kufikiria juu ya mtu anayeuliza swali la msomaji.

Pia napanga hapo mbele namna jinsi Mungu Alivyonionyesha ndoto hizo.

1. Ndoto ya kwanza: Nilimuona Khalifa wa kwanza anapita mbele yangu. Miti inasujudia upepo mkali unavuma nikauliza katika ndoto huyu ni nani? Sauti ilitokea katika ule upepo mkali ikisema ni Malaika. Nikashikwa na mshangao. Ndoto hiyo niliiona kabla sijajiunga na Jumuiya Ahmadiyya.
2. Ndoto ya pili: Niliona katika ndoto jua na mwezi vyote vinatoa mwanga mkali kupitia katika dirisha la nyumba yangu. Ndoto hii iliendelea kunitokea mara nyingi mpaka ikanibidi kwenda kwa rafiki yangu kumweleza ndoto yangu yeye akaniambia kuwa jua na mwezi kuona katika ndoto maana yake umemwona jini la wachawi, kazana kwenda kwa waganga ili kupata kinga. Lakini moyo wangu haukutaka kufanya hivyo lakini baadaye nikakutana na kiongozi wa Jumuiya Ahmadiyya akaniambia ukweli wa mambo kwamba jua ni Nabii*saw* na mwezi ni Masihi Aliyeahidiwa na ameshafika.
3. Ndoto ya tatu: Niliionyeshwa kitabu cha Qur'an Tukufu katika ndoto. Maonyesho hayo yalikuwa kama ifuatavyo: kulionekana mtu amesimama mbele yangu ameshika kitabu. Kitabu hicho ni Qur'an Tukufu. Amekifungua ananionyesha na kuniuliza kile alichoshika ni kitu gani? Nikamjibu kuwa hicho ni kitabu. Akaniuliza tena ni kitabu gani? Nikasema ni Qur'an Tukufu. Akaniambia soma. Mimi nikamjibu sijui kusoma Qur'an Tukufu, akaniambia utajua baadaye kisha akaondoka. Ndoto hii ilirudia rudia karibu mara nne kwa siku tofauti tofauti. Wakati huo wote mimi nilikuwa Mkristo wa Romani Katoliki, jina langu lilikuwa linaitwa Romanus Abeli Mbawala, Parokia ya Peramiho Kigungo Liganga ambapo Liganga kwa sasa ni Parokia.
4. Ndoto ya nne: Ndoto hii niliota kwamba siku ile ilikuwa Jumapili kwa hiyo mimi nilikuwa naenda kusali kanisani. Lakini nilipofika njiani pahala hapo nikakuta kimefungwa kitambaa. Nikaambiwa nichague herufi moja katika hizo mbili ninayoipenda. Aliyekuwa anasema maneno hayo alikuwa nyuma yangu yaani mgongoni kwangu akaniambia nisigeuke kumuangalia mpaka kwanza nichague herufi ninayoipenda. Nikauliza herufi hizi zina maana gani? Akanijibu kwanza uchague uipendayo ndipo nitakuambia maana ya herufi hizo. Nikachagua S. akaniambia umefanya vizuri sana, sasa geuka niangalie. Nilipogeuka alikuwa baba yangu mzazi ambaye muda huo alikwisha fariki. Muda wote huo nilikuwa Mkristo.
5. Mimi nilikuwa na mazoea ya kwenda kufanya ibada ya sala na maombi mbalimbali sehemu fulani ambapo moyo wangu ulinituma kufanya hivyo. Nilikuwa nafanya jambo hili kama siri na nilipenda mahala hapo. Nilikuwa namtoroka mke wangu na watoto na kwenda kuslai pale pahala. Nilisali sala za Kikristo lakini hakuna aliyejua jambo hili bali Mungu peke Yake. Ndoto ikanifika usiku wa Alhamisi kuamkia Ijumaa. Ndoto hiyo ilikuwa kama ifuatavyo:

Nikaona upepo mkali sana ambao katikati yake kulikuwa na kisulisuli. Upepo ule ulilenga katika nyumba yangu nikadhani utaezua nyumba yangu lakini haukuezua nyumba bali uliingia ndani na kunichukua. Nilibebwa ndani ya kile kisulisuli kikanipeleka kule porini nilikozoea kufanya ibada kwa siri. Kiliponifikisha kile kisulisuli pahala hapo kikaganda kisiende mbele wala nyuma. Mara sauti ikatoka ndani yake ikiniambia angalia chini yako kuna nini? Nilipoangalia nikaona kuna watu 6, kulia kwangu watu 3 na kushoto kwangu watu 3. Hapo ndipo palitokea jambo ambalo sikutegemea kuwa linaweza kutokea. Watu watatu wa kulia kwangu – Sheikh, Mwalimu, Maamuma. Watu watatu wa kushoto kwangu – Padre, Katekista, Muumini. Watu watatu wa kulia kwangu wamepanga altale ya mawe yaweza kuwa na upana wa mita 2 au 3, wa kushoto kwangu nao wamefanya vivyo hivyo. Nikasikia sauti inatoka katika kisulisuli inatamka wewe kuanzia leo utakuwa Muislam, jina lako MUSSA. Nikauliza kwamba sauti hii ni ya nani? Ikajibu mimi Mwenyezi Mungu, kwani mahala hapa patakatifu nilishusha Manabii Wangu zamani kwa siri lakini watu hawajui kuwa hapa ni patakatifu. Ningependa pajengwe nyumba ya kuabudia.

Wale watu sita hakuna aliyekuwa anazungumza na mwenzake. Basi ukiweza waambie watu wajenge nyumba ya kuabudia.

Kisulisuli kikanisogeza katika alta ya washeki na kunishusha penye alitale ile. Basi nikashituka nikawa macho nikasikia adhana ya asubuhi, pia siku ile ilikuwa ni siku ya Ijumaa. Ilipofika asubuhi nikaoga maji nikaenda msikitini kwa Sunni kwani nilikuwa nikiamini kuwa misikiti yote ni sawa kiimani kumbe kazi ilikuwa bado inaningoja mbele. nilipofika nikakaa pale nje hadi walipomaliza kuswali ndipo akatokea mzee mmoja jina lake Omari Mtiula ambaye ni msaidizi wa Sheikh Mpale kutoka Mtwara. Mzee Mtiula akaniuliza "unataka nini?" maana alijua kuwa mimi ni Mkristo wa Romani Katoliki. Nikamwambia "nina shida". Shida gani? Akauliza. Nikamjibu "naomba kukutana na Sheikh Mpale". Akaniuliza "wa nini"? Nikamjibu "nina shida ya kiroho", akasema "hebu niambie mimi". Nikaanza na zile ndoto za kwanza basi akasema usiendelee kusimulia maana wanapita watu wengi twende nyumbani kwangu. Akanipeleka hadi nyumbani kwake akaandaa chai na chapati mezani kwake kisha mazungumzo yakaanza. Nilipofikia katikati ya mzungumzo akasema basi usiendelee sana maana moyo wangu unashindwa kuvumilia kwa sababu mambo uliyoonyeshwa ni mazito ila nakusihi tu kwamba kwa Sheikh nitakupeleka lakini usimsimulie kwani ataona wivu na atakuharibia mambo yako bure ila ukasimulie tu kidogo kuwa unahitaji kusilimu na inatosha.

Basi tulipofika kwa Sheikh Mpale akanikabidhi kwake nikaanza kutoa kilichonileta kama alivyoniambia Mzee Mtiula. Nikahojiwa kuwa au kuna mwanamke ameniambia niingie Uislamu. Nikakataa, akanikabidhi kwa Mzee Mtiula anifunze baadhi ya mambo yya dua na mengineyo. Siku ile nikaanza kuswali na wakati mwingine wazee wa msikitini pale walikuwa wananipeleka nyumbani baada ya kuwali Isha. Basi mambo yakaanza. Ninakumbuka kuwa nilionyeshwa Qur'an Tukufu niisome, kwa kuwa sasa nipo msikitini basi niombe kujifunza kusoma. Palikuwa na mwalimu wa Madrasa lakini akaniambia kwa sababu wewe ni mtu mzima hutaweza kujifunza Qur'an. Hapo tena ikawa mtihani mkubwa kwangu lakini Mwenyezi Mungu Alinifanyia mpango kwa urahisi kama Alivyoniahidi katika ndoto kuwa nitajua kusoma Qur'an Tukufu baadaye. Sasa baadaye Mungu Akaleta muujiza bila yule Sheikh kujua. Muujiza ulikuwa hivi: Sheikh yule alikuwa na tabia ya kutukana Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya na kumkashifu Masihi Aliyeahidiwa as kufika. Mpango wake Sheikh alikuwa anatoa darsa baada ya Isha na kusema Makadiani wanapoteza watu na kuwapeleka motoni. Basi nikamwambia Sheikh, naomba unionyeshe hao Makadiani wako wapi nataka nikawaulize kwa nini wanafanya mambo hayo!? Siku ya kwanza akakata. Siku ya pili akakataa. Siku ya tatu akakubali, akanipa kijana anipeleke kwa Sheikh Rafiq Malik. Sheikh Mpale alinipa ilani kuwa nikishafika kwa Sheikh Malik nimuone mara moja niondoke nirudi tena kwake. Lakini mambo hayakuwa hivi. Baada ya kuonana na Sheikh Rafiq Malik na kunikaribisha ofisini kwake, macho yakatua kwenye picha ya Masihi Aliyeahidiwa as na picha ya Khalifa Mtukufu wa kwanza ra. Mwenyeji wangu alinipokea vizuri sana na nikamuuliza kuhusu kusoma Qur'an Tukufu anidushie naweze kusoma. Nikaanza kusoma siku ile ile. Baadaye nikaenda kuswali kule kule msikitini kwake. Jioni ile darasa halikuwepo. Aliniuliza je umewaona Makadiani? Nikasema sijawaona. Hukumkuta yule muhindi? Aliuliza. Yule nimemkuta lakini sijawaona Kadiani. Yule mhindi alikuambia nini? Nikamjibu ameanza kunifundisha kusoma Qur'an Tukufu. Akasema lakini kwa Qur'an wanafundisha vizuri. Nikamuuliza mbona ulisema wanamtukana Mtume? Pia wao wana Qur'an ya kwao? Sasa imekuwaje useme anafundisha vizuri? Basi baada ya muda mfupi **nikajiunga na Jumuiya mwaka 1975.**

Bustani ya Washairi

WAZAZI

1. Wazazi baba na mama, muwe na mapenzi mema
Haifai kutumbama, mtatuweka vilema
Ndoa yenu iwe njema, iliyojawa hekima
Wala msifarakane, mtaumiza watoto.

2. Muwe na kauli njema, mtujenge sisi hapa
Tuwe na kizazi chema, kama Mungu atatupa
Uchamungu jambo jema, sio jambo la kutupa
Wala msifarakane, mtaumiza watoto.

3. Meunganishwa na ndoa, tafadhari mpendane
Ndoa siitie doa, mkataka mgombane
Msiwaze kujitoa, msitamani ujane
Wala msifarakane, mtaumiza watoto.

4. Kuachana ni kubaya, na wala msijaribu
Hiyo tabia ni mbaya, inakubidi utubu
Nawasema bila haya, na wala siwasulubu
Wala msifarakane, mtaumiza watoto.

5. Mtaumiza watoto, mtapokuwa tofauti
Msione kama ndoto, kuuzunisha umati
Msifanye ya kitoto, mtaundiwa kamati
Wala msifarakane, mtaumiza watoto.

6. Mtaundiwa kamati, kuyaweka mambo sawa
Naomba mjidhatiti, mpendane sawa sawa
Nyweshaneni matikiti, mahaba yapate dawa
Wala msifarakane, mtaumiza watoto.

7. Wala msifarakane, kwa mambo madogo dogo
Sala tano mkazane, msivilambe visogo
Imeruhusiwa wane, ili kuepusha zogo
Wala msifarakane, mtaumiza watoto.

8. Nyie wazazi wapendwa, mtulee sawa sawa
Kufunzwa sio kudundwa, kutupiga na upawa
Tuwe sawa tumefundwa, tusije ota mabawa
Wala msifarakane, mtaumiza watoto.

9. Kazi kwetu watoto, tusiwagawe wazazi
Tusikolezee Moto, wakigombana wazazi
Sisi bado ni watoto, hatuujui uwazi
Wazazi wakigombana, mtoto usuluhishe.

10. Sisi hapa ni watoto, tufikirieni sana
Tutajapata mazito, wazazi wakitengana
Hayatafaa majuto, haifai kulumbana
Wazazi wakigombana, mtoto usuluhishe.

11. Mzazi wetu mmoja, atakujaza uongo
Ili tu muwe pamoja, akuharibu ubongo
Wala hatasema ngoja, atakubebesha bango
Wazazi wakigombana, mtoto usuluhishe.

12. Kisa mama kaachika, unaona kaonewa
Anasema kadhalika, unafiki kaumbiwa
Jiulize kwa hakika, hivi mambo yako sawa?
Wazazi wakigombana, mtoto usuluhishe.

13. Ewe baba tafadhali, mtoto umechukua
Usimjaze shubili, mama ake kumuua
Mfundhishe maadili, ayaishi akikua
Wazazi wakigombana, mtoto usuluhishe.

14. Watoto tujihadhari, kuegemea upande
Sote tuwe mahodari, tupende kila upande
Tusiweke kachumbali, mlo kaingia mende
Wazazi wakigombana, mtoto usuluhishe.

15. Napumzika kidogo, Akili imeshachoka
Nimekumbusha kidogo, tunapaswa kuyashika
Kuoa si jambo dogo, tupunguze heka heka
Wazazi wakigombana, mtoto usuluhishe.

Abdallah S. Kalindima (K-mtoto)
#MMAKONDE MSOMI
kalindimasenior@gmail.com

SALHA

1. Ndoa ni jambo la kheri, sote tunafurahia
Kwa kudura za Kahari, na leo yametimia
Dada Salha ghururi, mume umejitwalia
Subira ukiishika, Itadumu yako Ndoa.

2. Leo mesha funga ndoa, mekua bibi na bwana
Faraja metupatia, kwa wawili kuoana
Mwende huko kutulia, tulio kutulizana
Subira ukiishika, Itadumu yako Ndoa.

3. Sasa mambo ni shwari, kwako unajiendea
Haukutaka yasiri, hii suna ya nabia
Kweli umejisitiri, kwenye hii jumuia
Subira ukiishika, Itadumu yako Ndoa.

4. Ndoa yako ni safari, hakika wende salama
Isije kuwa kikiri, mwisho ikaja kuzama
Mambo yote ya ushari, yaepuke kwa karama
Subira ukiishika, Itadumu yako Ndoa.

5. Sije ukatoka kwako, bila mume kuridhia
Hata na wageni wako, awe anawatambua
Takuwa heshima kwako, Dada mimi nakwambia
Subira ukiishika, Itadumu yako Ndoa.

6. Tango pia fesibuku, hiyo nayo mitihani
Kuna watu na vikuku, mambo yote hadharani
Wala sitie shauku, kuishi mitandaoni
Subira ukiishika, Itadumu yako Ndoa.

7. Shemeji yetu Latifu, mola atakujalia
Kutunza hii turufu, daima sije potea
Kwa kudra za Raufu, kimwana umeopoa
Subira ukiishika, Itadumu yako Ndoa.

8. Ninakuomba wahadi, udumishe hii Ndoa
Mapenzi yao yazidi, watoto kuwajalia
Mafunzo ya Muhamadi , daima kuzingatia
Subira ukiishika, Itadumu yako Ndoa.

9. Mola Mjaze neema, ya akhera na dunia
Ya dini yako Karima, Dua ninakuombea
Usipatwe na zahama, na nyingi pia fedhea
Subira ukiishika, Itadumu yako Ndoa.

10. Dada Salha kipenzi, miko nishakupatia
We mtoto wa Azizi, Pawaga unatokea
Sisi Ng'amilo wapenzi, kheri tunakutakia
Subira ukiishika, Itadumu yako Ndoa.

Rajabu Abasi Mkieti.
Al Wattan _Mlezi
Lusanga Muheza Tanga

MDOMO

1. Kwa jinale Rahmani, Mlichopanda moyoni,
E mdomo kitu gani, Mtima na ufungua
Mavuno nawapatia, Nilichokuchukulia?
Utu wangu wanivua, Domo nimekosa nini?

2. Siku ya jana jioni Mengine nimesikia,
Katuhukai nyumbani, Kila uchao na njia,
Mdomo haya huoni, Kazi kunisingizia.
Utuwangu wanivua, Ewe domo unanini?

3. Limerefuka lisani, Kwa yangu kuhadithia,
Yani wewe huna soni, Uongo kusimulia,
Merna yangu huyaorii, Hayo ukawaambia
Utu wangu wanivua, Domo unataka nini?

4. Mkono wangu shavuni, Ninapokuangalia,
Na wewe sina imani, Kwa unavyo nifanyia,
Dhana mbaya sio fani, Acha kujibwabwajia,
Utu wangu wanivua, Mdomo kwa kisa gani?

5. Mazuri yake husseni, Domo hukuzingatia
Namba tisa uwanjani, Ahmad wa Kondoa
Wote waliyabaini, Ya domo wakanambia,
Utu wangu wanivua, Domo kwa nini lakini?

6. Sijitakasi moyoni, Wamia asilimia,
lla sababu sioni, Machafu kunitutia,
Ambayo hata ndotoni, Sijawahi fikiria,
Utu wangu wanivua, Domo wanitajiani?

7. Kuyasema mdomoni, maneno yenye hatia
Ambayo sijatamani, Jua ndo yako tabia
Usijigeuze kuni, Motoni utaingia,
Utu wangu wanivua, Domo kwani we shetani?

8. U lipyoto kisimani, Maji unayachafua
Kikulacho kinguoni, Jipu nimelipasua
Wapitia kwa mwandani, Njia unazotumia,
Utu wangu wanivua, Domo unapata nini?

9. Namaliza kwa huzuni, Ulidhani sijajua,
Yale mazuri ya Shani, Domo unayafumbia
Mambo ya kubunibuni, Uache nakuusia,
Utu wangu wanivua, Domo hupendi amani?

Mwl. Najat Fakim Said Nangolo
THE BIG BOSS
Mtiti Jamaat- Tanga

ZUHURA INAVYONG'ARA

1. Hasema tangu waali, ukadhani maskhara
Hiki sio kibatali, tazama inavyong'ara
Inawaka bulibuli, hanena hii Zuhura
Zuhura inavyong'ara, ina nuru kwelikweli

2. Tazama yake miali, iangazavyo surura
Mwanga wake ni mkali, giza sasa linagura
Chaonesha abrali, chafichua maayara
Zuhura inavyong'ara, ina nuru kwelikweli

3. Zuhura mwanga aali, twaonyeshwa vya kukera
Kila kitu ki dhahili, kinacholeta madhara
Na kila kitu kilichoghili, kinadakwa kwa kamera
Zuhura inavyong'ara, ina nuru kwelikweli

4. Mng'aro wafika mbali, umetandawaa bara
Kisiwani wakubali, ndo waleta hongera
Hakika siyo batili, hii ni ile Zuhura
Zuhura inavyong'ara, ina nuru kwelikweli

5. Yakhe hii si chemli, mwanga umetia fora
Ni zaidi ya kandili, mafuta yake fikara
Si koroboi asili, hii ni ile Zuhura
Zuhura inavyong'ara, ina nuru kwelikweli

6. Utapoteajie hali, mwangaza upo hadhara?
Kila njia na mahali, paonekana jahara
Yamulika mulimuli, hii bwana ni Zuhura
Zuhura inavyong'ara, ina nuru kwelikweli

7. Enyi wenye tamthil, wa hekima na busara
Chatosha hiki kalili, msigongeshe vipara
Mwalijua jambo hili, wala halina harara
Zuhura inavyong'ara, ina nuru kwelikweli

Al Ustadh Mhenga Khamisi S.S. Wamwera
Kimbangulile – Mbagala Rangi Tatu
Dar us salaam.

Usafi
ni Sehemu ya Imani



Hadithi yangu pendwa ni, "Anna-Nazafat Minal-Iiman" ambayo inamaanisha "**Usafi ni sehemu ya imani**". Hadithi hii inanifundisha umuhimu wa kuwa msafi na kukifanya chumba changu safi. Kama ninakuwa na nguo chafu zikitapakaa kwenye sakafu ya chumba changu na ikatokea mtu kuja atasema, "angalia chumba chako! Sio kisafi. Kichafu kweli kweli".



Kama sisafishi kinywa changu basi mdomo wangu utanuka vibaya na watu hawatataka kukaa nami au kuongea na mimi. Kibaya zaidi ya hicho ni kwamba meno yangu yatatoboka na kung'oka.



Kama siogi kila siku basi nitaanza kutoa harufu mbaya na nywele zangu zitakuwa zinateleza na zenye vumbi.

Je kuna yeyote atataka kuwa rafiki yangu kama siwi msafi?

Mtume Mtukufu Muhammad (amani iwe juu yake) alitupendelea sana kwa kutupa muongozo huu na nitahakikisha naufuata. Pia naenda kumweleza mama na baba umuhimu wa hadithi hii na nilichojifunza.

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno yafuatayo kwa kuyazungushia na Penseli

KALIMA	JUZUU	ANKABUT	HUZUR	ILHAM
SHAHADA	MALI	CHANDA	KUSOMA	MAAKULI
WASAA	YAKUBU	AITAMAD	TAFSIR	MAUUD
TABIA	ARABU	MAJLIS	TAJWID	RAMADHAN

S	T	A	J	W	I	D	H	M	U	R	U	A
Y	T	A	F	S	I	R	A	Z	A	U	M	D
A	A	R	D	D	M	H	D	M	Z	Z	A	M
R	M	K	M	A	L	I	I	U	T	N	U	V
A	K	A	U	I	K	L	J	T	A	N	U	G
B	U	P	A	B	A	H	G	H	B	S	D	T
U	S	H	L	K	U	Q	D	M	I	K	U	D
T	O	R	U	X	U	A	P	L	A	B	A	N
Q	M	B	F	Z	M	L	J	W	A	M	B	W
N	A	D	L	A	U	A	I	K	A	H	X	R
X	L	Z	R	W	M	R	N	T	J	S	T	M
S	H	A	H	A	D	A	I	V	V	M	A	L
R	D	M	H	N	T	A	C	H	A	N	D	A

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta za picha hapo chini ili upate picha moja iliyokamilika.



Majibu ya Chemsha Bongo la Toleo la Machi: *Hongereni mliopatia yote*

Ngamia - A'raaf, An Naml
Farasi - An Nahl
Kondoo - Al An'aam
Kunguru - Al Maaida
Nyuki - An Nahl
Nyani - Al A'raaf
Tembo - Al Fiil
Nyangumi - Al Qalam
Punda - An Nahl
Nguruwe - Al An'aam
Buibui - Ankabut
Mbwa - Al A'raaf
Nyumbu - An Nahl
Mbuzi - Al An'aam

Khuddam Shinyanga Watoa Damu Wasafisha Zahanati



Vijana wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Mkoa wa Shinyanga wakifyeka nyasi katika zahanati ya Nhelegani.

Na **Mtandao**

Viongozi wa Jumuiya ya Waislam wa Viongozi wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Mkoa wa Shinyanga (Ahmadiyya Muslim Jamaat Mkoa wa Shinyanga) wakiongozwa na vijana wa Jumuiya hiyo wamejitolea kuchangia damu ili kuokoa maisha ya mama na mtoto katika Zahanati ya Nhelegani iliyopo katika kata ya Kizumbi Manispaa ya Shinyanga.

Zoezi hilo la uchangiaji damu limefanyika Alhamis ya Aprili 11, 2019 ambapo mbali na kuchangia damu vijana hao wamesafisha mazingira katika zahanati hiyo kwa kufyeka nyasi na kuzoa taka.

Rais wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Mkoa wa Shinyanga, Ndugu Yusuph Mgeleka alisema wameamua kuchangia damu ili kunusuru maisha ya mama na mtoto lakini pia kufanya usafi ili kuweka mazingira ya zanahati ya Nhelegani kuwa salama.

Naye Mwalimu wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Mkoa wa Shinyanga, Yusuph Gesonko alisema zoezi la kuchangia damu ni huduma kwa viumbe ijulikanayo kama 'Khidmat Khalqi' ikiwa ni utekelezaji wa kauli mbiu ya Ahmadiyya ya '***Upendo kwa wote bila chuki kwa yeyote***'.

Mbeya Waadhimisha Siku ya Masihi Aliyeahidiwa



Kutoka uk. 1

Sheikh wa BAKWATA Mbeya, Sheikh Ally Mwansasu ambaye katika hotuba yake huku akiashiria kwenye bango ambalo lilikuwa na maandiko ***Mwislam ni yule ambaye wengine wanasalimika kwake kwa mkono wake, ulimi wake na matendo yake*** alisema "maneno haya ni tafsiri ya kauli ya bwana wetu mtume Muhammad*saw* na tafsiri hii ni sahihi zaidi iliyotolewa kwa ufasaha na utaaluma wa kina kabisa na hii ni sifa maalum ya Waahmadiyya kwamba tafsiri zao zinakuwa sahihi kabisa wala hazitolewi bila ya utafiti mkubwa wa lugha". Kisha Naibu wa Mstahiki Meya wa Jiji la Mbeya alifuatia na Mchungaji wa kanisa la Moravian Jimbo Kuu la Kusini Magharibi aliyemwakilisha Askofu Mkuu wa kanisa hilo alimalizia.

Mgeni wa heshima katika hafla hiyo ambaye alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbeya Mjini, Mh. William Paul Ntinika alishangaza wahudhuriaji kwa kuanza hotuba yake kwa kughani shairi liloimbwa na Mwl Makarani Hamza Balama katika ufunguzi kisha akaongezea beti za kwake kwa sauti mwanana sana. Kisha akanasihi juu ya kuendeleza amani iliyopo na umoja baina yetu licha ya tofauti zetu za imani na itikadi.

Mara baada ya hotuba hiyo ya mgeni rasmi, Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry alitoa hotuba fupi akiwashukuru wageni wote kwa ujio wao na uvumilivu na kisha akawakumbusha wanajamaat kukumbuka na kushikamana na masharti ya ba'iat na kuyaishi kila siku.

Ugawaji wa zawadi za vitabu kwa baadhi ya wageni ulihitimisha hafla hiyo ambayo ilipata kurushwa mubashara na Redio Ahmadiyya Mtwara na kuchukuliwa na vyombo vya habari vingine yakiwemo magazeti 2, redio 2 na TV 2.

Lajna Kitonga Wafanya Waqal Amal ya Nguvu



Kutoka uk. 1

Gah kwa ajili ya maombi ya pamoja, hata hivyio tawi la Jalsa Gah ndio waliokuwa wenyeji wa msafara huo. Lajna hao walifanya shughuli mbalimbali kwenye zahanati hiyo zikiwemo kulia, kufagia pia kudeki vyumba vyote bila kuacha hata kimoja.

Aidha uongozi wa zahanati hiyo ulifurahishwa sana na kitendo hicho pia waliwapongeza washiriki wote na kuwakaribisha tena kwa moyo mkunjufu kwani hiyo ni zahnati yao, pia waliomba waendeleze utaratibu huo.

Ikumbukwe kuwa zahanati hiyo ndiyo pekee inayowahudumia wananchi wa Kitonga. Aidha Mganga Mkuu wa zahanati hiyo aliongea na wanafunzi waliokuwepo hapo na kuwashauri wapende masomo hasa ya Sayansi kwani dunia tuenda nayo ni ya sayansi na teknolojia.

Allah Awajaalie moyo wa kupenda kusaidia viumbe Wake na waendeleze utaratibu wa usafi sehemu yoyote iwayo. Amina.

Je Wajua?

Ahmadiyya Wanaruhusiwa Kushiriki Siasa

Akitolea jibu suala hili, Huzur aqdas alisema: *"Kama raia unayo haki ya kutafuta nafasi ya kisiasa na kama Waislam wa Ahmadiyya watakuwemo katika siasa inaweza kusaidia kupatikana kwa mazingira yenye haki na usawa na watakuwa na mchango wa moja kwa moja katika namna serikali inavyoendeshwa. Ukiangalia huko nyuma kabla ya sheria zinazowapinga Waahmadiyya Pakistan, Waislam wa Ahmadiyya kadhaa walichaguliwa katika mabunge na bila shaka Chaudhry Zafrullah khan sahib alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Pakistan. Kwa hivyo, kama ukitaka kuingia katika siasa endelea, waweza kufanya hivyo."*

Mambo mawili tunajifunza kutoka kwenye jibu hili murua :

1. Ahmadiyya ambao wanajiunga kwenye siasa wana jukumu la kuwa waadilifu na watenda haki katika harakati zao za kisiasa.

2. Ahmadiyya ambao wanajiunga na siasa **hawawezi kuwa watazamaji**. Aidha uingie **kuongeza thamani** kwa kutoa **michango madhubuti** au **ukae mbali**.

Hali ya watu ambapo wanajiingiza katika siasa ili tu kunufaika na ***mgao wa keki ya taifa*** si chaguo la Kiahmadiyya kabisa.

Allah Atuwezeshe tuwe wenye kuufuata muongozo wa Khalifa wa zama hadi mwisho wetu, Amin.

MATUKIO KATIKA PICHA





Matukio ya Maadhimisho ya Siku ya Masihi Aliyeahidiwa[as] na Mkutano wa amani mkoani Mbeya





Matukio ya Maadhimisho ya Siku ya Masihi Aliyeahidiwa[as] na Mkutano wa amani mkoani Mbeya



Vijana wa Ahmadiyya wakichangia damu.



Mganga katika zahanati ya Nhelegani,Johanes Barnabas akiendelea na zoezi la kuwapima presha vijana wa Ahmadiyya waliojitolea kuchangia damu.



Viongozi pamoja na vijana wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Mkoa wa Shinyanga baada ya kumaliza kufanya usafi katika zahanati ya Nhelegani.



Rais wa Mkoa wa Shinyanga, Ndugu Yusuph Mgeleka, Qaid Ilaqa ya Shinyanga, Abdulghani Msimba na Mwalimu wa Mkoa wa Shinyanga, Mwl Yusuph Gesonko wakitoa zawadi ya soda, maji na sabuni kwa wagonjwa katika zahanati ya Nhelegani.

Ukweli Kuhusu 'Uchawi' Juu ya Mtukufu Mtume^{saw}

Kutoka uk. 11

maana yake sio kwamba sawa na uelewa wao sio alikuwa amerogwa. Bali mradi wake ni kuwa watu wanasema kuwa amerogwa. (Alifanyiwa uchawi) na lengo la ru'ya ile halikuwa jingine zaidi ya hili kuwa kitu kile ambacho wale watu wabaya walikificha na kukitumbukiza kisimani, na kwa njia hii walikuwa wanawadanganya wenzao. (walikuwa wanadanganya watu waliokuwa kama wao, walikuwa wanaivumisha, na wanaeneza habari hii miongoni mwa wanafiki), kile kitu Allah akidhihirishe kwa Mtume wake ili uchawi ule uliotungwa auangamize. Hivi ndivyo ilivyotokea kwamba vifaa vya uchawi ule viliangamizwa, na kisima kilifukiwa. Na moja kwa moja kutokana na matokeo yake ile fikra ya Mtume^{saw} kuwa hawa wanataka kudanganya watu wa kawaida, ilitoweka.

Ahadi hii ya Allah ilitimia kwa nguvu zote kuwa;

(Hatashinda mchawi yeyote popote au wakati wowote atakapokuwepo)

Yaani mchawi yeyote hataweza kumshinda Nabii kwa kutumia njia iwayo yoyote.

Kwa neno zima kutokana na hadithi ya hapo juu mambo yafuatayo yanathibitika:

Ya kwamba baada ya tukio la Sulh Hudaibiyya ambalo kwa sababu yake Mtume^{saw} ilibidi apate wasiwasi kwa sababu ya fikra ya kupotea watu wengine. Naye alikuwa baadhi ya wakati anasahau mambo ya kawaida yaliyohusiana na mambo ya nyumbani.

Jambo la pili ni kwa kuangalia hali hii ya Mtume^{saw} mayahudu na wanafiki waliokuwa wanatafuta fursa kupitia mambo kama haya ya kufedhehesha na kudhalilisha dini ya kiislam na mwanzilishi wake mtakatifu, walianza kueneza jambo hili kwa siri kuwa sisi tumemroga Nabii wa dini ya kiislam, (Mungu apishe mbali). Uvumi wao huu ni sawa na ule uliotokea katika vita vya Banu Mustaliq kwa sababu ya kuachwa nyuma kwa Hadhrat Bi Aisha^{ra} walikusudia kumfedhehesha yeye, na kwa njia hii walijaribu juhudi zao hizi chafu kuleta shida katika maisha ya Mtume^{saw}

Jambo la tatu ni hili kwamba, Kama ya dhahiri ya uchawi huu uliotungwa ili watu wa kawaida waweze kudanganywa kwa urahisi zaidi, watu hawa wenye tabia mbaya kupitia kwa Labid bin Al-A'asam mnafiki mwenye asili ya kiyahudi sawa na kawaida yao walifunga baadhi ya nywele vifundo katika kitana na kuzika katika kisima, na wakaanza kuzungumza kwa siri, iliyokuwa sababu ya mfadhaiko wa Mtume^{saw}

Jambo la nne ni kwamba wa sababu ya jambo hili Mtume^{saw} aliomba kwa unyenyekevu mkubwa dua kwa Allah kwamba "Ee Allah fitna hii uimalize kabisa kwa fadhili zako, na udhihirishe kwangu hakika yake haswa, ili mimi niweze kuikomesha na kuwaokoa watu wa kawaida. Hivyo kwa sababu ya kupokelewa kwa dua mambo yote yakadhihirika.

Jambo la tano ni kuwa Allah alipokea dua zake zile, na kudhihirisha ushenzi wa Labid bin Al-A'asam, ambapo Mtume^{saw} akiwa na mashahidi kadhaa akaenda kule kisimani, na kitana kile kukizika, si hayo tu bali hata kisima chenyewe alikifukia, ili kusibaki ishara yake wala alama ya aina yoyote.

Lakini mwisho linajitokeza swali moja kwamba Mtume^{saw} aliyekuwa Nabii mwenye heshima kubwa, mbora kuliko manabii wote, na Khaatam-un-nabiyyiin, kwa nini alipata ugonjwa wa kusahau, ambao unaweza kuwa ni kikwazo cha utekelezaji wa majukumu ya unabii? Kwa hiyo katika jawabu lake mtu anatakiwa azingatie kuwa kila Nabii ana hali mbili, upande moja anakuwa Nabii na Mtume wa Allah sababu ambayo inamfanya apate bahati ya kuzungumza na Allah, na kuwa mwalimu kwa wafuasi wake katika maswala yote ya dini, naye anakuwa mfano kwao, na kwa upande mwingine yeye ni mwanaadamu miongoni mwa wanaadamu wengine, naye anaguswa na kufata hali zote za kimaumbile ya kibinaadamu na kuathirika na hatari zote za kimaumbile, ambazo zinawagusa wanaadamu wengine. Ndiyo maana Allah katika Qur'an Tukufu Amemwambia Mtume^{saw} kuwa;

Yaani "Ewe Mtume^{saw}! waambie watu kuwa mimi ni mwanaadamu kama ninyi (nami nafuata kanuni zote za kimaumbile ambazo zinawahusu watu wengine). Naam mimi ni Mtume kutoka kwa Allah nami nimejaaliwa ufunuo kutoka kwa Allah kwa ajili ya mwongozo wa wanaadamu. Hii ni tafsiri yake ya kimaelezo.

Katika aya hii latifu hali mbili za manabii zimeelezwa kwa namna iliyo bora kabisa. Yaani wao upande moja wametofautishwa na wanaadamu wengine, na kwa upande wa pili hawakuweza kutoka nje ya mstari waliokuwemo watu wengine. Basi yule mtu anayefikiria kuwa manabii na mitume wako nje ya kawaida ya kimaumbile na hatari zake basi huyo ni mwongo. Bila shaka manabii vilevile wanakuwa wagonjwa kama wanavyokuwa watu wengine. Hadhrat Mian Bashir Ahmad^{ra} ameandika kuwa manabii wanaweza bali wamekuwa wakiathirika na magonjwa yafuatayo; malaria, taifod, T.B. homa, mafua, kukohoa, ugonjwa wa mifupa, maumivu ya kichwa, maumivu ya misuli, ugonjwa wa kuzidi kwa hisia, kufadhaika, huzuni, kukirihika, kusahau, kupata ajali, majeraha, kuumizwa n.k. (katika kugusia tunatakiwa kuzingatia kwamba mambo haya yaliyotajwa yanajulikana kutokana na hadithi na historia kwamba alifariki kwa homa ya tumbo (taifod)). Isipokuwa kama kwa fadhili za Allah kama kuna Nabii yeyote aliyenusurika na ugonjwa fulani kwa ahadi maalum. Kama sehemu hii mtu apate swali kwamba Qur'an inasema juu ya Mtume^{saw} kuwa;

(Yaani Sisi tutakufundisha elimu nawe hautaisahau). Basi katika jawabu lake mtu anatakiwa atambue sawa sawa kuwa ahadi hii ni kuhusu wahyi wa Qur'an pekee, na sio mambo ya kawaida. Mradi wake ni kuwa "Ewe Mtume^{saw}! wahyi tuliokuteremshia kwa ajili ya mwongozo wa umma, wewe huo hautousahau, nasi tutauhifadhi mpaka kiyama. Ahadi hii haihusu mambo ya kawaida ya kila siku, mambo ya kidunia na yale mambo ambayo kwa dhahiri yanahusiana na dini. Kwa hiyo inathibitika kutoka katika hadithi kuwa Yeye s.a.w katika sehemu nyingi alikuwa anasahau sawa na hali ya kimaumbile, bali katika hadithi inasemwa pia kuwa Yeye^{saw} wakati wa kuongoza swala alisahau idadi ya rakaa haswa za swala husika, na alikumbuka baada ya kukumbushwa na watu. Hadithi hii inapatikana katika kitabu vyote viwili cha Bukhari na Muslim. Na kuna sehemu zingine nyingi Mtume^{saw} alikuwa anasahau.

Bali katika Hadith Mtume^{saw} amewahi kusema kuhusu yeye mwenyewe kuwa;

Yaani mimi ni mwanaadamu kama ninyi ninasahau kama mnavyosahau, basi ninaposahau jambo fulani nikumbusheni.

Basi kama Mtume^{saw} baadhi ya wakati alikuwa anasahau kwa muda, vile vile baada ya tukio la Sulh Hudaibiyya kwa muda fulani alipata hali ya kusahau katika sura ya ugonjwa. Basi haya ndiyo maelezo sawa na riwaya inayohusu uchawi yaliyotolewa na baadhi ya maulamaa waliopita. Kwa mfano Allama Maazariyyi anasema;

Kwa ajili ya ukweli wa Mtume^{saw} kuna dalili madhubuti chungu nzima, na miujiza yake kadhaa ambayo ni dalili ya ukweli wake. Na mambo ya kawaida ya dunia ambayo hakutumwa kwa ajili yake, kuhusu mambo hayo hii yatatambulika kama hali ya ugonjwa kama vile mwanaadamu mwingine anavyoathirika na magonjwa ya kawaida.

Na Allama Ibn-ul-Kassaar anasema kuwa:

Mtume^{saw} ile hali ya ugonjwa iliyompata, huu ulikuwa ni ugonjwa sawa na magonjwa mengine kama ilivyodhihirika katika maneno haya ya mwisho ya hadithi kwamba "Allah ameniponyesha. (jambo hili limeelezwa waziwazi ndani yake.)

Almuradi kwa neno zima kwamba baada ya tukio la Sulh Hudaibiyya hali iliyokwishatajwa ya Mtume^{saw} ambayo iliyosemwa kuwa ni matokeo ya uchawi wa maadui, aslan abadan hayakuwa matokeo ya uchawi, bali yalikuwa ni hali ya kusahau iliyotokana na hali halisi iliyotokea. Ulikuwa ugonjwa wa kawaida wa kusahau, ambao baadhi ya watu waenezaji wa fitna walitunga propaganda hii dhidi ya dhati takatifu ya Mtume^{saw} Qur'an tukufu inatupilia mbali visa yote vya uchawi dhidi ya manabii, inapinga kabisa. Akili ya kawaida ya mwanaadamu inakataa kuikubali. Maneno ya hadithi yanabatilisha maelezo haya yanayotungwa juu yake. Na daraja la Mtume mbora wa manbii^{saw} inakifunua na kukiweka wazi kisa hiki cha uchawi.

Hadhrat Mirza Bashir Ahmad^{ra} pia amegusia jambo hili kwamba si jambo lisilokuwa na faida kwamba kama ilivyokuja riwaya ya Hadhrat Khalifa wa pili Allah Amsaidie (anazungumzia kipindi kile alipokuwa bado yu hai). Riwaya hii inapatikana katika ukurasa wa 75 jalada la kwanza la kitabu cha Sirat-ul-Mahdi, kuwa safari moja Baniani mmoja adui mkazi wa Gujrat, alifika Qadian. Naye alikuwa ni mtaalamu wa kiini macho (Hypnotism). Yeye alifika katika mkutano wa Masihi Aliyeahdiwa^{as} na kimya kimya pole pole akaanza kufanya kiini macho kwake, ili kusababisha yeye kufanya baadhi ya harakati mbaya ili aweze kumfanyia mizaha kwa watu ili wamcheke, lakini wakati Masihi Aliyeahidiwa^{as} alipogeuka kwake, yeye akakimbia huku akipiga kelele. Na pindi alipoulizwa kwamba kumetokea nini kwako? Akajibu kuwa mimi nilipo mfanyia kiini macho Mirza sahib (Masihi Aliyeahidiwa a.s), basi mimi niliona kana kwamba kuna simba mkali aliyesimama mbele yangu ambaye alitaka kunirarua, nami niliogopa na kukimbia. Yeye^{ra} anaandika kwamba Yeye (Masihi Aliyeahidiwa^{as}) ni mtumishi wa Mtume^{saw} ikiwa hii ndiyo daraja ya mtumishi, sembuse kufikiria kuhusu bwana wake yaani kuhusu Mtume^{saw} kwamba yeye (Mungu apishe mbali) aliathirika na uchawi wa kiini macho wa myahudi, jambo hili linawezekana kukubalika namna gani?

Mwishoni ninasoma baadhi ya semi za hakimu mwadilifu wa zama (Masihi Aliyeahidiwa^{as}) ambazo ni muhimu zaidi katika maelezo yote.

Mtu mmoja katika kikao chake fulani alimuuliza kuwa "nini ni maoni yako kuhusu uchawi wa makafiri waliyomfanyia Mtume^{saw}?" Masihi Aliyeahidiwa^{as} akajibu akasema kwamba uchawi pia unatoka kwa shetani. Hii sio shani ya manabii na mitume ya kwamba wao waathirike na uchawi wowote. Bali uchawi ukiwaona unawakimbia na kutoka. Kama vile Allah anavyosema;

Kwamba "angalieni kulikwepo na uchawi dhidi ya Nabii Musa^{as} lakini Je, mwishoni Nabii Musa hakuwa mshindi? Jambo hili ni kosa kwamba uchawi ulishinda dhidi ya Mtume^{saw} Sisi hatuwezi kukubali. Kuamini kitabu cha Bukhari na Muslim kwa kufumba macho yetu jambo hili ni kinyume na itikadi yetu. Akili haikubali jambo hili ya kwamba uchawi umuathiri Nabii huyu mwenye shani ya hali ya juu. Mambo haya kwamba kutokana na athari ya uchawi kumbukumbu ya Mtume^{saw} ilipotea, hili limefanyika na lile limefanyika, haliwezi kuwa sawa katika hali yoyote ile.

Kisha yeye^{as} anasema, "inafahmika kuwa mtu fulani mbaya alitengeneza jambo hili mwenyewe. Ingawa sisi tunaiangalia hadithi kwa heshima zote, lakini hadithi ile inayokwenda kinyume na Qurani, hiyo inakwenda kinyume na heshima ya Mtume^{saw} sisi tunawezaje kuiamini. Wakati ule ulikuwa wa kukusanya hadith. Ingawa wao (yaani wale waliozikusanya hadithi) walizikusanya hadithi kwa uangalifu, lakini hawakuwa na umakini wa kutosha. (ingawa walionesha uangalifu mkubwa) ule ulikuwa ni wakati wa kukusanya, lakini sasa ni wakati wa kuchambua na kufikiria (kile kilichosahihi). "Angalia na tafakari vizuri. Hadith ambayo inapingana na Qur'an au heshima ya Mtume^{saw}, hadithi hiyo ni ya kuachana nayo, au itakuwa ina maelezo mengine (kama vile alivyofanya Hadhrat Mirza Bashir Ahmad Sahib^{ra} au Hadhrat Kalifat-ul-Masih wa pili^{ra}). Kisha Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa^{as} anasema, "kukusanya hadithi za nabii^{saw} ni kazi yenye thawabu." (yaani kukusanya hali ya maisha na shughuli za manabii ni kazi yenye thawabu) lakini hili ni jambo la kawaida kwamba wanaokusanya hawawezi kufanya kazi kwa umakini mkubwa. Kwa hiyo ni hiyari ya kila mtu ya kwamba afanye kazi hii kwa tafakuri na umakini mkubwa. Yale mambo ambayo mtu anaweza kuyaamini, ayaamini. Na yale anayoweza kuyaacha ayaache. Jambo kama hili kwamba Mtume^{saw} alifanyiwa uchawi (Mungu apishe mbali) yanafanya imani itoweke. Yeye anasema kuwa "Allah anasema:

"Pindi watu wadhalimu wanaposema kwamba ninyi mnafuata mtu yule aliyekwisharogwa, aliyefanyiwa uchawi, aliyeathirika na uchawi."

Watu hawa wanaosema maneno haya ni wadhalimu sio Waislamu. Kauli hii ni ya wale wasiokuwa waaminifu na wadhalimu kuwa Mtume^{saw} (Mungu apishe mbali) alirogwa na kuathirika na uchawi. Hawa hawafikirii kuwa kama hali hii ni ya Mtume^{saw} (Mungu apishe mbali) basi umma wake utakuwa na hali gani? Utakuwa umeteketea kabisa.

Sisi hatujui kumetokea nini kwa watu hawa kwamba wanazungumza vibaya kuhusu hali ya Mtume^{saw} ambapo yeye ni Nabii Mtakatifu yule ambaye Manabii wote waliopita wamemhesabu kunusurika na mguso wa shetani.

Tunamshukuru Allah kwamba sisi baada ya kumuamini Imamu wa zama hizi, tumekuwa watu tunaofahamu na kuelewa vizuri daraja la Mtume^{saw}.

Ukweli Kuhusu 'Uchawi' Juu ya Mtukufu Mtume^{saw}

Inatoka uk 12

amekwishazifanya wakati alikuwa bado hajazifanya. Au katika baadhi ya wakati alikuwa anadhania kwamba alikwishaenda kwa mke wake fulani wakati hakika haswa alikuwa bado hajaenda. (naye katika maelezo yake anasema kwamba) Kuhusiana na jambo hili inatakiwa kuzingatia kuwa hii ilikuwa ni kawaida ya Mtume^{saw} kwamba sawa na sharia za dini ya kiislam yeye^{saw} alikuwa ameweka mpangilio wa zamu kwa wake zake na kila siku jioni alikuwa anakwenda katika kila nyumba ya mkewe mmoja kumjulia hali, na mwisho alikuwa anafika kwenye nyumba ya mke yule ambaye siku ile ilikuwa zamu yake. Riwaya iliyokuja juu inaashiria jambo hili. (Kwa neno zima riwaya hii inaendelea mbele). Mwisho Allah kwa kupitia ru'ya alidhihirisha hakika ya fitna hii kwa Mtume^{saw} n.k.

Huu ndiyo muhtasari wa tukio hili ambao imekwishaelezwa katika tafsiri ya Hadhrat Musleh Mau'ud^{ra} Hii ni riwaya ya Imam Bukhari^{ra} ambayo muhtasari wake yeye^{ra} ameeleza.

Kisha anaandika tena kwamba huu ni muhtasari wa riwaya ile ambayo iliyotajwa katika baadhi ya vitabu vya historia na hadith. Riwaya hii imezungukwa na visa mbalimbali vilivyozushwa kiasi kwamba kujua uhakika wake haswa ni vigumu. (yaani kuna visa vingi vilivyozushwa kuhusu riwaya hii kiasi hiki kwamba inakuwa vigumu kujua ukweli wake.) Yeye^{ra} anaandika. "Kama riwaya zote zitakubaliwa basi (Allah apishe mbali) dhati yake takatifu na iliyobarikiwa itathibitika kuwa yeye^{saw} (kinywa changu kijae mchanga) alikuwa ni mtu mwenye hali dhaifu sana kiasi kwamba adui wake mbaya aliweza kumtia katika hali yoyote ya hatari kwa njia ya uchawi wake. Na kwamba yeye (adui wake) kwa kumfanya Mtume^{saw} kuwa shabaha ya mazingaombwe (na uchawi) wake aliweza kudhibiti utendaji wa akili na moyo wake kiasi kwamba alishindwa kujinasua nafsi yake na uchawi huu. (Kama riwaya hii ielezwe kwa jinsi ilivyoelezwa katika hadithi na historia, basi matokeo yake yatakuwa haya ambayo ni mabaya sana. Jambo hili haliwezekani.) Lakini badala yake kama kuhusiana na riwaya hizi tafakari ifanyike kwa kuzingatia mantiki na hali halisi, na kwa kuzingatia uchambuzi wa riwaya yenyewe, (yaani uchunguzi na utafiti ufanyike) basi itadhihirika wazi kuwa hii ilikuwa ni kwa sababu ya maradhi ya kawaida ya kusahau tu ambayo kwa sababu ya tafakuri kubwa ya baadhi ya wakati na matokeo yake ya udhaifu wa mwili ilitokea kwake kwa muda mfupi, ambayo maadui wenye nia mbaya walifaidika nayo na kusambaza habari kuwa sisi tumemfanyia uchawi Nabii wa dini ya kiislam (Allah apishe mbali). Badala yake Allah Alimjaalia Mtume^{saw} afya njema mapema na kutia masizi katika sura ya maadui, na uzushi wa uwongo wa wanafiki ukaangukia kwenye wumbi na kupotea.

Yule aliye mshindi wa nguvu kubwa za kishetani na mbora wa mitume wote^{saw} ambaye ni mwenye kusaga tikitiki nguvu za kishetani ambaye dunia haijapata kumshuhudia mwingine zaidi yake na wala hatatokea mtu wa aina hii mwingine hapo baadae, kuhusiana naye kufikiria kuwa aliweza kuwa shabaha ya uchawi wenye nguvu ya kishetani wa mtu dhalili mwenye asili ya kiyahudi, haya yatakuwa ni matumizi mabaya ya mwisho ya akili ya binadamu. (Jambo hili haliwezi kufikiriwa). Na haya sio madai yetu tu bali Mtume^{saw} (nafsi yangu iwe sadaka kwake) mwenyewe amelipinga. Ufafanuzi wake unatoka katika hadithi moja. Hadhrat Bi Aisha^{ra} akasema kuwa, Ewe Mtume wa Allah! Je, mimi ninaye shetani? Mtume^{saw} akajibu ndiyo. (Hadhrat Bi Aisha^{ra} akamuuliza Je, mimi ninaye shetani? Akamjibu, Ndiyo). Mimi nikamuuliza je, kila mtu ana shetani pamoja naye? Yeye^{saw} akajibu, Naam. Hadhrat Bi Aisha^{ra} akashangaa na kusema Ewe Mtume wa Allah! Je, hata wewe kuna shetani pamoja nawe? Yeye^{saw} akamjibu, Ndiyo, lakini Allah amenijaalia udhibiti juu ya shetani wangu kiasi kwamba yeye amekuwa Mwislamu.

Je, mbele ya kuwepo kauli hii ya Mtume^{saw} iliyowazi na bayana mtu anaweza kufikiria jambo hili kuwa myahudi fulani mnafiki ambaye sawa na Qur'an tukufu ni miongoni mwa mataifa yaliyolaaniwa alimfanya Mtume^{saw} yaani yule mtu aliye mbora, shabaha ya uchawi wake kwa msaada wa shetani wake. Naye^{saw} kutokana na athari ya uchawi wenye nguvu ya shetani, kubaki katika mfadhaiko, wasiwasi na mgonjwa?

Watu waongo wameendelea katika kila zama kutumia mbinu mbaya na za uwongo dhidi ya haki. Lakini Allah mwenye nguvu mwenye heshima Ameendelea kuwadhihirisha waongo wa aina hii. Kama vile anavyosema:

Yaani Allah Amekwishaandika na kuamua kwamba katika zama za kila Mtume wangu Mimi na mitume wangu tutashinda. Na hakuna mbinu yoyote ya kishetani itakayofaulu katika kushindana nasi.

Yeye^{ra} anazidi kuandika, "Kisha kuna suali hili linaloibuka kwamba nini hakika ya tukio hili lililoelezwa mpaka katika kitabu cha hadith cha Sahih Bukhari kwa kauli ya Hadhrat Bi Aisha^{ra} Kama tutaitafakari kwa kuzingatia habari iliyotajwa mbele na nyuma na kuzingatia tabia na mwenendo wa mayahdi na wanafiki, basi kugundua hakika ya tukio hili haiwi kazi ngumu tena. Kitu cha kwanza ni kwamba ni lazima tujue kuwa tukio hili la uchawi lililotungwa na kubuniwa lilitokea baada ya tukio la mapatano la Sulh Hudaibiyya. Katika Tabaqaat ibn-e-Sa'ad imeandikwa, ambapo Mtume^{saw} kutokana na Ru'ya aliyoiona aliamua kwenda Makka kwa nia ya kufanya Umra, naye alifika huko, lakini kwa sababu ya Maquraishi kumzuia njiani, kwa dhahiri ilionekana kuwa alishindwa kutimiza nia yake na kurudi. Kushindwa huku kulikoonekana ilikuwa ni huzuni kubwa, ilikuwa ni kawaida kwamba makafiri na wanafiki kufanya mzaha na kulaumu mpaka baadhi ya Waislamu wakweli na wenye nia njema kama inavyokuja katika hadith kuwa mtu mkubwa kama Hadhrat Umar^{ra} kwa sababu ya kushindwa huku akababaika kwa muda. Jambo hili limeandikwa pia katika kitabu cha Bukhari. Riwaya hii ya Hadhrat Umar^{ra} ni hadithi ya kitabu cha Bukhari. Kutokana na hali hii na kwa sababu ya hofu kuwa baadhi ya Waislamu walio dhaifu wangeteleza, kulitokea athari kubwa katika hali ya kiafya ya Mtume^{saw} naye^{saw} kwa muda mrefu alikuwa na wasiwasi mwingi, na ni lazima athari ya fikra hii iligusa hali yake ya kiafya. Na Mtume^{saw} katika wasiwasi huu muda mwingi alikuwa anaomba dua kwa Allah, kama vile ilivyogusiwa katika maneno ya hadith (**Da'aa wa Da'aa**) n.k. ili tukio la Sulh Hudaibiyya isiwe sababu ya kusimama kwa muda maendeleo ya dini ya kiislam. Dua hii ilikuwa ni ya aina ile ile ya siku ya Badr ambapo yeye Mtume^{saw} pamoja na kupata ahadi ya ushindi kutoka kwa Allah lakini kwa kuona nguvu ya maadui aliomba;

(Ee Allah! Kama utaliangamiza kundi hili wewe hutaweza kuabudiwa katika ardhi hii katu).

Kutokana na sabau hizi kulitokea athari katika viungo vya mwili wake na nguvu za kuhifadhi. Naye^{saw} alipatwa na hali ya kusahau sahau kwa muda. (Katika baadhi ya riwaya hali hii ilibaki kwa muda wa siku mbili tatu au siku mbili au siku moja na usiku mmoja tu. Lakini kwa neno zima iwe muda wa siku zozote, kiasi fulani cha athari alikipata ambayo ilikuwa ya lazima. Hadhrat Mirza Bashir Ahmad Sahib^{ra} ametoa tathmini hii kuwa athari hii ilikuwa kwa siku chache, na hii ilikuwa ni kwa sababu ya fikra nyingi alizokuwanazo, na kwa sababu ya udhaifu wa imani ya waislamu alikuwa na hofu kubwa). Hii ni hali ya kawaida ya kibinaadamu ambayo manabii wa Allah hawakunusurika. Pindi mayahudi na wanafiki walipoona kuwa Mtume^{saw} siku hizi anaumwa na kwa sababu ya udhaifu wa mwili na akili amepata ugonjwa wa kusahau, basi wao sawa na kawaida yao kwa nia ya kueneza fitna wakaeneza habari kuwa sisi tumemroga Nabii wa waislam (Allah apishe mbali) na kwamba hali hii ya kusahau imetokana na athari ya uchawi ule ule. Na wao sawa na desturi yao ya toka zamani ili kuonesha alama ya dhahiri, wakazika kwenye kisima kitana kilichofungwa mafundo kadhaa ya nywele.

Pindi taarifa ya uchawi uliotungwa ilipofika kwa Mtume^{saw} akaomba zaidi kwa Allah dua ili kumaliza fitna hii. (kama vile Hadhrat Aisha^{ra} alivyokwishasema kuwa baada ya kupata taarifa hii aliomba dua kwa bidii); na akafanya maombi kwa Mola wake wa mbinguni kwamba Yeye Ampe taarifa kamili ya majina ya wale walioizusha fitna hii na hali halisi ya namna ya uchawi huu ulivyotungwa, ili aweze kudhihirisha hakika ya uchawi huu wa uwongo. Hivyo Allah Akasikia dua zake za unyenyekevu na kumfunulia uhakika haswa kwa kupitia ru'ya.

Na usemi wa msingi wa Qur'an

(Yaani hakuna mchawi katika sura yoyote ile atakayefaulu mbele ya manabii hata kama akishambulia kwa njia yoyote na upande wowote.) Kisha kwa kuzingatia uamuzi huu wa mwisho wa Qur'an;

Yaani "Wadhalimu wanasema ninyi hamumfati ila mtu tu aliyerogwa."

Katika Qur'an imeandikwa kuwa makafiri wamesema kauli hii hii. Matokeo ya kuyatafakari maneno ya hadith, na namna inavyozungumza, na kwa kuzingatia misemo ya Kiarabu, riwaya hii ya kitabu cha Bukhari itaeleweka kama ni usemi wa mtu mwingine. Yaani usemi wa mtu mwingine maana yake ni kwamba mtu anayezungumza anajifanya anazungumza kuhusiana na yeye mwenyewe wakati hakika yenyewe ni kwamba watu wengine ndio wanaosema hivi. Yaani anaeleza habari za mtu mwingine. Kwa hiyo maana ya riwaya hii itakuwa kama hivi kwamba Hadhrat Bi Aisha^{ra} anasimulia kuwa wakati fulani Mtume^{saw} alifanyiwa uchawi (Yaani maadui walieneza habari za uwongo kwamba yeye^{saw} amerogwa.) Hadhrat Bi Aisha^{ra} hakusema hivi mwenyewe. Tafsiri yake itakuwa hivi kwamba maaudi wameeneza taarifa hii kuwa yeye^{saw} amerogwa mpaka wakati mwingine alikuwa anafikiri kuwa kazi fulani amekwishafanya wakati alikuwa bado hajafanya. Na katika riwaya nyingine imeelezwa kuwa baadhi ya wakati alikuwa anafikiri kwamba yeye amekwishakwenda kwa mkewe fulani wakati ambapo alikuwa hajaenda nyumbani kwake. Katika siku hizi sawa na ufafanuzi wa Hadhrat Bi Aisha^{ra} "Siku moja yeye alikuwa nyumbani kwangu naye alikuwa akiomba dua kwa Allah mara kwa mara katika mfadhaiko mkubwa. Baada ya kuomba dua hii Yeye akaniambia; Ewe Aisha! Je, wewe unajua kuwa Allah ameniambia jambo lile ambalo mimi nilimuomba? Mimi nikamuuliza, Ewe Mtume wa Allah^{saw}! Hilo ni jambo gani? Yeye^{saw} akajibu (katika ndoto) watu wawili walikuja kwangu (au katika hali ya kashf). Mmoja alikaa karibu na kichwa changu na mwingine karibu na miguu yangu. Kisha kati yao mmoja akamuuliza mwingine mtu huyu ana matatizo gani? Hadhrat Mirza Bashir Ahmad Sahib^{ra} anaandika kwamba namna ya kuzungumza pia ni kana kwamba usemi unaomuhusu mtu mwingine mwenyewe, inaashiria mazungumzo kumhusu mtu mwingine, na baadaye ni mazungumzo yale yale marefu yaliyokwishapita kwamba matatizo yake ni haya kuwa myahudi fulani amemfanyia uchawi, na watu wanasema hii ni athari yake. Kisha Hadhrat Bi Aisha^{ra} anasema; baada ya ndoto au kashf hii Mtume^{saw} alienda kwenye kisima kile pamoja na baadhi ya maswahaba zake na kufanya uchunguzi. Pale kulikuwepo baadhi ya miti ya mitende (yaani kilikuwa kisima chenye kina kirefu). Kisha yeye^{saw} akarudi kwa Hadhrat Bi Aisha^{ra} na akamwambia; Ee Aisha mimi nimekwishakiangalia. Maji ya kisima kile yanaendelea kuwa mekundu kama maji ya hina (ilikuwa ni kawaida ya mayahudi ili kuwadanganya watu kama ilivyokwishaelezwa, walikuwa wanatia rangi ya maji ya kisima cha aina hii) na miti yake ya mitende ilikuwa inaonekana mibaya kama miti ya mipungate. Hadhrat Aisha^{ra} anasema; mimi nikamuuliza Mtume^{saw} kwamba kwa nini hujatoa kitana kile na kukitupa nje? Sehemu nyingine inasemwa; kwa nini hukuchoma? Yeye^{saw} akajibu Allah Amenihifadhi, na Akaniponya, sasa kwa nini mimi kwa kutupa nje nieneze habari yake mbaya kwa watu? (kutokana nayo kulikuwa na hofu ya kuibuka kwa fikra ya uchawi miongoni mwa watu waliokuwa na tabia dhaifu). Basi kisima kile kilifukiwa na kukiziba kabisa.

Hadhrat Mirza Bashir Ahmad Sahib^{ra} anaandika ikumbukwe kwamba usemi wa mtu mwingine (yaani pindi jambo fulani kwa niaba ya mtu mwingine linaposemwa, au kauli ya watu wengine inapotajwa kwa watu wengine), mtindo wa kuzungumza kwa namna hii ulikuwa desturi ya Waarabu, bali hata katika Qur'an tukufu aina hii ya mazungumzo yametumika. Hivyo sehemu moja Allah akiwaambia watu wa motoni anasema;

Yaani ewe yule mtu uliyetiwa kwenye jahannum! Onja adhabu hii ya Allah. Bila shaka wewe ni mheshmiwa na mtu mwema sana.

Sehemu hii haina maana kwamba Allah Anawahesabu watu wa motoni kama waheshimiwa na wema (Allah apishe mbali). Bali sawa na usemi wa mtu mwingine maana yake ni hii; Ewe mwanadamu, ambaye mwenzake na yeye mwenyewe alikuwa anajihesabu mheshimiwa (baada ya kufanya mambo mabaya duniani walijihesabu kuwa sisi ni waheshimiwa sana) sasa wewe onja utamu wa adhabu ya Allah. Namna hii hii wale watu wawili au malaika walitumia kwenye ru'ya katika mazungumzo yao walioonekana na Mtume s.a. katika ru'ya. Ndiyo maana waliposema mtu huyu amerogwa

Endelea uk. 10

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

Mapenzi ya Mungu

RAJAB - SHA'BAN 1439 AH | APRILI 2019 | SHAHADAT 1398 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu*saw*

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Hurairah r.a. aliyesema ya kwamba Nabii s.a.w. alisema: Asiyeachana na kuongopa na kudanganya, Mwenyezi Mungu Hana haja ya kwamba yeye mtu huyo aache chakula chake na kunywa kwake. (**Bukhari**)

Ukweli Kuhusu 'Uchawi' Juu ya Mtukufu Mtume*saw*



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akihutubia Ijumaa katika msikiti wa Baitul Futuh uliopo jijini London nchini Uingereza ambapo hotuba yake hurushwa mubashara kupitia satelaiti duniani kote kupitia MTA.

Baada ya Tashahhud,Taawwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Amir ul Momeneen, Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a alisema:

Hadhrat Qais bin Mihsan alikuwa miongoni mwa maswahaba wa kianswaar (Maswahaba wenyeji wa Madina) wa Mtume*saw* Katika baadhi ya riwaya jina lake linafahamika kama Qais bin Hisn. Yeye ametokana na kabila la maanswaar la Banu Zuraiq. Jina la mama yake ni Aniisa bint Qais, na baba yake ni Mihsan bin Khalid. Yeye alishiriki katika vita vya Badr na Uhud. Miongoni mwa mabinti zake yupo Umm-e-Sa'ad bint Qais. Yeye alipofariki watoto wake walikuwa Madina.

Swahaba mwingine ni Hadhrat Jubair bin Iyaas. Jina la baba yake ni Iyaas bin Khalid. Yeye alishiriki katika vita vya Badr. Yeye alitokana na tawi la Banu Zuraiq la kabila la Khazraj. Hadhrat Abdullah bin Muhammad amesema kuwa yeye (Jubair) alikuwa anaitwa Jubair bin Ilyaas. Na katika riwaya nyingine imeelezwa kuwa jina lake ni Jabar bin Iyaas.

Katika hadithi inaelezwa kuwa myahudi mmoja alimfanyia Mtume*saw* uchawi, ambapo Mtume*saw* aliathirika. Na inaelezwa kwenye riwaya nyingine kuwa alifanya uchawi kwenye kitana na nywele na kutumbukiza kwenye kisima cha Zirwaan. Na Mtume*saw* baadae alikwenda kuvitoa. Inasimuliwa katika kitabu cha maelezo ya Sahih Bukhari iitwayo Fath-ul-Baari kwamba kitana na nywele zile ziliondolewa na Hadhrat Jubair bin Iyaas kutoka katika kisima cha Zirwaan. Na sawa na simulizi zingine zilitolewa na Hadhrat Qais bin Mihsan.

(*Fath-ul-Baari kutoka kwa Imam Ibn-e-Hajar, kitab-ut-twib, baab al-Sihr, Hadith 5763, J 10, Uk 282, kilichochapishwa na kampuni ya Qadimi Kutub Khana, Karachi.*)

Ndiyo maana mimi nimewaweka maswahaba hawa wawili pamoja. Katika hawa yeyote yule aliyevitoa si jambo la msingi sana. Jambo haswa ni hili kuwa Je, athari ya uchawi ilikuwapo juu ya Mtume*saw*? Ukweli haswa ni upi? Nini maoni yetu kuhusiana na jambo hili? Nasi ni wajibu kwetu kujua jambo hili. Yaani kama kuna jambo lolote la lawama juu ya dhati ya Mtume*saw* au watu wanamlaumu, ni wajibu wetu kuyatolea jawabu. Kwa hiyo mimi sasa nitajaribu kuyatolea maelezo ambayo yanapatikana katika vitabu vya Jamaat. Leo mambo haya yenye mnasaba na maswahaba hawa wawili nitayatolea maelezo.

Hadhrat Musleh Maud*ra* akitoa utambulisho wa maelezo wa surat-ul-Falaq huku akizungumza juu ya tukio hili anasema, yeye anazungumza juu ya surah hii kwamba baadhi ya watu wanafikiri kuwa Surat-ul-Falaq na Surat-un-Naas sura hizi zote za mwisho ziliteremka Makka. Wengine wanazitaja kuwa ni za Madina yaani zilifunuliwa Madina. Yeye*ra* anaandika: "Wale watu wanaosema kuwa sura hii iliteremka Madina dalili zao ni kwamba hii na ile iliyokuja baada yake ilihusika na ugonjwa ule wa Mtume*saw* ambao ulifikiriwa kuwa wayahudi walimfanyia Mtume*saw* uchawi. Wakati ule sura hizi mbili zikateremka. Naye Mtume*saw* alizisoma na kujipulizia." Mambo haya yanaelezwa na yeye*ra* kwamba haya yanasemwa. Na mufassiriina wanasema kwa kuwa tukio hili lilifanyika Madina basi sura hizi mbili ziliteremka Madina. Kwa neno zima upendeleo umepewa wazo hili kwamba sura hizi zote mbili ni za Madina - yaani zimeteremshwa Madina. Hadhrat Musleh Maud*ra* anaandika hivi kwamba: Haya ni moja ya maoni ya mufassiriin, sio ushahidi wa kihistoria. Ingawa hatuna ushahidi wa hakika wa jambo hili ambalo litatufanya sisi kusema kuwa sura hii ni ya Makka. Ingawa pia ile sababu iliyoelezwa ni ya hovyo, "yaani sababu ya kipuuzi." Kwa sababu hata kama ingekuwa imeteremka Makka, Mtume*saw* pia angeisoma na kujipulizia. Basi kufikiria kujipulizia pekee kuwa ni sababu ya kuteremka kwa sura hii Madina, hii sababu sio sahihi."

"… Kuumwa kwa Mtume*saw* na watu kufikiria kuwa kulitokana na uchawi wa wayahudi juu yake, maneno yaliyosimulia tukio hili ni haya yafuatayo. "Hadhrat Musleh Maud*ra* ameandika maneno haya wakati akizungumzia utambulisho wa sura hii. Yeye anaandika, "Kwa sababu mufassiriina, riwaya ya Hadhrat Bi Aisha*ra* wameipa kipaumbele, kwa hiyo sisi tunatoa tafsiri ya riwaya ile ile tu." Imesimuliwa kutoka kwa Hadhrat Aisha*ra* kwamba Mtume*saw* alifanyiwa uchawi kutoka kwa mayahudi, na athari yake ilifikia kiwango kikubwa hivi kwamba wakati mwingine Mtume*saw* alielewa kwamba kazi fulani ameifanya wakati alikuwa bado hajaifanya. Mchana mmoja au usiku mmoja Mtume*saw* aliomba dua. Aliomba dua tena akaomba dua. Kisha akasema: Ewe Aisha! Allah amenipa yale yote niliyoyaomba katika dua. Hadhrat Aisha*ra* anasema, mimi nikamuuliza hicho ni kitu gani. "ulichoomba? Allah amekupa nini wewe?" Mtume*saw* akajibu, "Watu wawili walifika kwangu. Mmoja alikaa karibu na kichwa changu, na mwingine karibu na miguu yangu. Kisha yule aliyekaa karibu na kichwa changu akamuambia yule aliyekaa karibu na miguu yangu au huenda alisema (Hadhrat Aisha anasema; huenda amesema haya) "Yule aliyekaa karibu na miguu akamuambia yule aliyekaa karibu na kichwa, kwamba mtu huyu (Yaani Muhammad Mtume wa Allah)"*saw* "ana shida gani? Mwingine akajibu kuwa amerogwa. Yule akauliza, nani aliyemroga? Yule akajibu, Labid bin al-A'asam myahudi. Ndipo yule wa kwanza akauliza, amerogwa wapi? Mwingine akamjibu amerogwa kwenye chanuo na nywele za kichwani ambazo zilikuwa katika kole la tende. Wa kwanza akauliza vitu hivyo viko wapi? Mwingine akajibu viko kwenye kisima cha Zirwaan. Hadhrat Bi Aisha*ra* anasema baada ya hapo Mtume*saw* na maswahaba zake*ra* wakaenda kisimani. Kisha wakarudi ndipo aliposema, Ewe Aisha! Naapa kwa Jina la Allah!! Maji ya kisima yalionekana kana kwamba ni maji mekundu yaliokamuliwa kutoka katika hina. Hadhrat Musleh Maud*ra* amelielezea tukio hili kwamba (inaonekana kuwa ilikuwa ni desturi katika wayahudi kwamba walipokuwa wanamroga mtu fulani walikuwa wanatia hina au kitu kingine cha aina yoyote katika maji ili kuonesha kwamba maji hayo yamekuwa mekundu kutokana na nguvu ya uchawi). Walikuwa wanafanya mbinu za kawaida kuwadanganya watu wengine wa kawaida, na yeye*ra* tena akawaambia watu kuwa tende za sehemu ile zilikuwa za aina hii "Mtume*saw* anasema" kama vile shetwani yaani vichwa vya nyoka (hapa makole ya tende yamenasibishwa na vichwa vya nyoka, kwa maana ya kwamba tende zilikuwa za makole) Hadhrat Bi Aisha*ra* anasema, mimi nikasema Ewe Mtume wa Allah! Kwa nini wewe hukuchoma vitu vile vilivyofanyiwa uchawi? Mtume*saw* akajibu, kwa kuwa Allah alikwishanijaalia ponyo kwa hiyo mimi sikupenda kufanya jambo ambalo litasababisha shari ya aina yoyote… ndiyo maana mimi nilitoa amri ya kuzika vitu hivyo. Kwa hiyo vilifukiwa. Hadhrat Musleh Maud*ra* anaandika kuhusu riwaya hii ya Hadhrat Bi Aisha*ra* kuwa "watu wawili wanaosemwa kuja kwa Mtume*saw* inaonekana kuwa walikuwa malaika wawili walioneshwa kwa Mtume*saw* Kama wangekuwa ni watu wangeonekana pia kwa Bi Aisha*ra* "yeye*ra* anasema" riwaya ile iliyosimuliwa kutoka kwa Hadhrat Bi Aisha*ra* maana yake ni hii tu kwamba Allah alimpasha habari Mtume*saw* kwa njia ya malaika kwamba mayahudi wamemfanyia yeye uchawi, maana yake sio hii kuwa kama inavyoaminika athari ya uchawi ndivyo ilivyotokea kwa Mtume*saw* kuwa nguvu ya uchawi ilimuathiri yeye Mtume*saw* "kisha anasema*ra* tena, Kwa neno zima" … pindi Mtume*saw* alipotoa vitu vile vya uchawi na kuvizika ardhini basi Wayahudi wakadhani kuwa uchawi walioufanya haukufanya kazi "ulikwisha." Hapa vilevile Allah Alimjaalia afya njema. Kwa ujumla Wayahudi walikuwa wanaamini kwamba wao walimfanyia Mtume*saw* uchawi (walimroga) ndio maana fikra yao iliwapeleka kwenye kuamini kuwa Mtume*saw* atakuwa mgonjwa. Yeye*ra* anaandika kuwa "katika riwaya hii pale unapodhihirika uadui wa wayahudi dhidi ya Mtume*saw* vile vile vivyo hivyo ndiyo inavyodhihirika hakika kuwa Mtume*saw* alikuwa Nabii mkweli wa Allah, kwa sababu yeye alipewa elimu kamili ya mambo haya kutoka kwa Allah kuwa wayahudi walikuwa wanamfanyia uadui. Kwa hiyo kujua kwake kwa mambo ya ghaibu (mambo ya badaae) na kushindwa kwa kusudio la mayahudi ni dalili iliyo wazi na yenye nguvu ya ukweli wa utume wake.

Kwa neno zima Hadhrat Musleh*ra* jinsi alivyotoa matokeo ya tathmini yake hii ndiyo hakika pekee kwamba mayahudi walimfanyia Mtume*saw* sawa na maoni yao lakini athari yake haikumpata Mtume*saw* na ule ugonjwa wa kusahau au mwingine wowote, kuna uwezekano wa kuwa na sababu nyingine. Lakini Allah baada ya kumpasha Mtume*saw* harakati hii ya mayahudi aliifanya ishindwe waziwazi dhana yao ya kuwa wamemroga Mtume*saw* Na wayahudi ile furaha walioipata katika maoni yao baada ya kuona ugonjwa wa Mtume*saw* au katika kueneza habari hii, ya kuzungumza kwamba hii ni athari ya uchawi wetu iliyosababisha ugonjwa huu unaoendelea. Hakika yake imeshadhirika.

Kisha katika vitabu vyetu kuna makala moja ya Hadhrat Mirza Bashir Ahmad Sahib*ra* ambamo kuna uchambuzi wa kina wa kitaaluma na wa kihistoria ambayo ina ufafanuzi zaidi wa tukio hili. Yeye*ra* anaandika;

Katika historia bali mpaka katika hadithi imesimuliwa kwamba baada ya mapatano ya Sulh Hudaibiyya mnafiki mmoja mwenye asili ya kiyahudi aitwaye Labiid bin Al-a'asam alimfanyia Mtume*saw* uchawi (au mazingaombwe), (Allah apishe mbali). Na uchawi huu ulifanyika katika sura ya kwamba kwenye kitana kimoja kwa kufunga kifundo cha nywele na juu yake kufanya kisomo (cha uchawi) na kutumbukiza kwenye kisima kimoja. Na inasemekana (Yaani yeye*ra* ndiye anayesema inasemekana) kwamba yeye*saw* alikaa katika athari ya uchawi huu kwa muda mrefu (Allah apishe mbali). (Jambo hili wao walilieneza sana). Katika kipindi hiki yeye*saw* muda mwingi alibaki katika hali ya huzuni na mfadhaiko. Na katika hali hii ya mfadhaiko alikuwa anaomba dua mara kwa mara, na katika hali hii sehemu yake kubwa iliyowazi ni kwamba katika siku hizo alikuwa na tabia ya kusahau sahau sana. (alikuwa anasahau baadhi ya mambo). Kiasi kwamba wakati mwingine baadhi ya kazi alikuwa anazihesabu kana kwamba

Endelea uk. 11

Shura ya Kitaifa na Uchaguzi uk. 4